**HUDUMA YA URAIA NA UHAMIAJI YA AYALANDI**

**OFISI YA ULINZI WA KIMATAIFA**

# Kijitabu cha Maelezo kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa

**TAFADHALI SOMA MAELEZO YOTE KWENYE KIJITABU HIKI KABLA UANZE KUJAZA DODOSO LAKO LA ULINZI WA KIMATAIFA**

## Lengo la kijitabu hiki

Kijitabu hiki cha maelezo kitakusaidia kuelewa utaratibu wa kuchakata maombi ya ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi. Kitakufafanulia pia haki na majukumuyako na utakuwa ukihusika na nani wakati wa mchakato huu wa maombi, uchunguzi na mapendekezo/uamuzi. Kijitabu hiki pia kinatoa maelezo kuhusu kupata kibali cha kusalia nchini kwa sababu nyingine.

## Ujumbe Muhimu

Unastahili kuweka kijitabu hiki cha maelezo ili uweze kukirejelea wakati maombi yako yanapokuwa yakichakatwa.

Wakati unaomba ulinzi wako wa kimataifa, unaingia katika utaratibu wa kisheria. Hati unazohitaji kukamilisha na maelezo unayohitaji kutoa kama sehemu ya mchakato wa maombi, uchunguzi na mapendekezo/uamuzi ni muhimu kwa mchakato huu. Kwa hivyo, ni muhimu sana kwamba usome maelezo yafuatayo kwa ukamilifu na utafute ushauri wa kisheria kama inavyohitajika ili uweze kuunga mkono maombi yako. Lazima ushirikiane na Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO). Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kuwa na matokeo mabaya ya kisheria kwa matokeo ya maombi yako.

Sheria inayosimamia uchunguzi na uamuzi wa maombi ya ulinzi wa kimataifa na hata pia kibali cha kusalia nchini na kuungana na familia yako nchini Ayalandi imewekwa katika Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa 2015 (Sheria ya 2015) na katika amri na kanuni zilizowekwa chini ya Sheria hiyo. Unaweza kupata sheria hii kamili kwenye tovuti zifuatazo www.inis.gov.ie na www.ipo.gov.ie.

Madhumuni ya kijitabu hiki ni kutoa maelezo na ushauri tu. Kijitabu hiki si ushauri wa kisheria na hakitoi tafsiri ya kisheria ya Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa 2015. Kama unahitaji maelezo zaidi kuhusu Sheria ya 2015 na athari zake kwa kesi yako, unastahili kutafuta ushauri wa kisheria.

Wakati juhudi zote zimefanywa ili kuhakikisha kuwa yaliyomo kwenye kijitabu hiki ni sahihi, hatutawajibika kwa makosa au upungufu wowote uliyo hapa ndani. Aidha, hakuna chochote katika kijitabu hiki kinastahili kuchukuliwa kama uwakilishi au ahadi ya jukumu lolote linalofunga la kisheria kwa sehemu ya Waziri wa Sheria na Usawa ('Waziri') au mhusika mwingine yeyote, ikiwa ni pamoja na maafisa na wahudumu wa Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa, kwa jukumu lolote linalozidi majukumu yaliyowekwa na sheria.

Ofisi ya Ulinzi wa KimataifaHuduma ya
Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi
Januari 2017

## Yaliyomo

**Sehemu ya 1 Ulinzi wa Kimataifa ni nini na ninawezaje kutuma maombi yangu?**

*1.1 Je, ulinzi wa kimataifa ni nini?*
*1.2 Ni nani anayeweza kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa?*
*1.3 Je, kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa ni hatua nzuri ya kuchukua katika hali yangu binafsi?*
*1.4 Ni wapi ninastahili kutuma maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?*
*1.5 Ni nani atashughulikia maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?*
*1.6 Kibali cha kusalia ni nini na ninawezaje kutuma maombi yangu?*
*1.7 Je, kuungana na Familia ni nini?*

**Sehemu ya 2 Maneno Muhimu**

*2.1 Je, Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa ni nini (IPO)?*
*2.2 Je, Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa ni nini (IPAT)?*
*2.3 Waziri ni nani?*
*2.4 Je, ni nani anayechukuliwa kama mkimbizi?*
*2.5 Je, ni nani anayefaa hifadhi mbadala?*
*2.6 Je, madhara makubwa ni nini?*
*2.7 Je, makatazo ya kurejeshwa nchi ya nyumbani ni nini?*
*2.8 Je, ni nani haruhusiwi kupata ulinzi wa kimataifa?*
*2.9 EURODAC ni nini?*
*2.10 Je, Eneo la Kawaida la Usafiri ni nini?*

**Sehemu ya 3 Mchakato wa Ulinzi wa Kimataifa**

*3.1 Ninastahili kutarajia nini wakati ninapoomba ulinzi wa kimataifa?*
*3.2 Ni hatua zipi za kwanza katika mchakato huu wa maombi?*
*3.3 Ukubalifu wa maombi yangu utabainishwa aje?*
*3.4 Ikiwa tayari nimepokea uamuzi wa maombi ya awali ya ulinzi wa kimataifa, ninaweza kutuma maombi mengine (maombi ya kufuatia)?*
*3.5 Je, mahojiano ya mwanzo ni nini?*
*3.6 Je, alama zangu za vidole na maelezo mengine ya biometriki yatachukuliwa?*
*3.7 Je, nitapokea maelezo yaliyoandikwa kuhusu mchakato wa ulinzi wa kimataifa?*
*3.8 Je, ninastahili kubeba nini wakati ninatuma maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?*
*3.9 Je, Cheti cha Makazi ya Muda (TRC) ni nini na nitakipokea lini?*
*3.10 Je, nikiwa mlemavu au niwe na mahitaji maalum?*
*3.11 Je, ninaweza kuomba ulinzi wa kimataifa nikiwa mfungwa au kizuizini?*
*3.12 Ni hali gani ambazo mwombaji wa ulinzi wa kimataifa anaweza kufungwa?*
*3.13 Je, ni nini hufanyika ikiwa nina watu wanaonitegemea chini ya umri wa miaka 18?*
*3.14 Je, ni wapi ninaweza kupata ushauri wa kisheria?*
*3.15 Je, ninaweza kuondoa maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?*

## Sehemu ya 4 Mahojiano na Uchunguzi

*4.1 Je, ni nini ninastahili kutarajia katika mahojiano yangu ya ulinzi wa kimataifa?*
*4.2 Je, ninaweza kumleta mtu yeyote kwa mahojiano yangu ya ulinzi wa kimataifa ili kunisaidia?*
*4.3 Na ikiwa siwezi kuhudhuria mahojiano au nishindwe kuhudhuria mahojiano yangu?*
*4.4 Je, nina jukumu la kushirikiana na mchakato wa maombi na matokeo yake ni gani nikishindwa kufanya hivyo?*
*4.5 Je, mchakato mkuu wa uchunguzi ni upi, pamoja na mahojiano ya kibinafsi?*
*4.6 Je, ni nini hufanyika baada ya mahojiano yangu?*
*4.7 Je, ni matokeo gani yanayowezekana ya maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?*
*4.8 Je, ni nini hufanyika kama sijapokea mapendekezo ya maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa katika miezi 6?*

## Sehemu ya 5 Rufaa na Ulinzi wa Kimataifa

*5.1 Je, nina haki ya kukata rufaa pendekezo la kutonipa ulinzi wa kimataifa na mapendekezo mengine?*
*5.2 Ninawezaje kukata rufaa?*
*5.3 Je kuna kikomo cha muda wa kuwasilisha maombi ya rufaa?*
*5.4 Je, nina haki ya kupata uwakilishi wa kisheria kwa maombi yangu ya rufaa?*
*5.5 Itachukua muda gani kusikiliza maombi yangu ya rufaa?*
*5.6 Ni wapi ninaweza kupata maelezo zaidi kuhusu mchakato wa rufaa?*

### Sehemu ya 6 Taarifa ya Hadhi ya Ukimbizi au Hifadhi Mbadala

*6.1 Je, ni nini hufanyika baada ya kupokea pendekezo?*

### Sehemu ya 7 Haki Zako ikiwa Utapewa Ulinzi wa Kimataifa

*7.1 Je, haki zangu ni zipi kama nitapokea ulinzi wa kimataifa?*

### Sehemu ya 8 Haki na Majukumu Yako katika Mchakato wa Ulinzi wa Kimataifa

*8.1 Je, haki zangu ni zipi katika mchakato wa maombi ya ulinzi wa kimataifa?*
*8.2 Je, majukumu yangu ni yapi katika mchakato wa maombi ya ulinzi wa kimataifa?*

### Sehemu ya 9 Watoto Wasiokuwa na Wazazi

*9.1 Je, ni nini hufanyika nikitafuta kuomba ulinzi wa kimataifa kama mtoto asiyekuwa na wazazi?*
*9.2 Je, ni utaratibu upi kama TUSLA - Shirika la Watoto na Familia litatuma maombi ya ulinzi wa kimataifa kwa niaba yangu?*
*9.3 Je, ni utaratibu gani unaotumiwa kumwelekeza mtoto chini ya umri wa miaka 18 kwa Bodi ya Usaidizi wa Kisheria (LAB)?*

**Sehemu ya 10 Kanuni za EU Dublin**

*10.1 Je, Kanuni za EU Dublin ni nini?*

**Sehemu ya 11 Chaguo za Kurejea kwa Hiari**

*11.1 Je, nina chaguo la kurejea nchi yangu ya asili/nchi ya makazi yangu ya zamani kwa hiari?*

**Sehemu ya 12 Maelezo Mengine**

*12.1 Je, ni taratibu zipi zinazotumika za kuipa kipaumbele maombi ya ulinzi wa kimataifa?*

*12.2 Je, ni nini kitakachofanyika kwa maelezo ninayoyatoa kwa Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa?*

**Sehemu ya 13 Kibali cha Kusalia**

*13.1 Ninawezaje kuomba kibali cha kusalia?*
*13.2 Ni maelezo gani muhimu kwa uamuzi wa Waziri kama atanipa au hatanipa kibali cha kusalia Nchini (Ayalandi)?*
*13.3 Ni nini hufanyika kama nitanyimwa kibali cha kusalia?*
*13.4 Ni nini hufanyika kama nitapewa kibali cha kusalia?*
*13.5 Je "mapitio" ya kunyimwa kibali cha kusalia hufanya kazi aje?*
*13.6 Je, ni nini hufanyika kama nitapewa kibali cha kusalia lakini niamue kukata rufaa pendekezo hilo la ulinzi kutoka kwa IPO hadi kwa IPAT?*
*13.7 Ni nini hufanyika kama nitanyimwa kibali cha kusalia baada ya mchakato wa mapitio?*

**Sehemu 14 Kuungana na Familia**

*14.1 Je, kuungana na Familia ni nini?*
*14.2 Je, kuna kikomo cha muda?*
*14.3 Mwanafamilia ni nani?*
*14.4 Ni maelezo gani ambayo ni lazima niyajumuishe kwenye Fomu ya Maombi ya Ulinzi wa Kimataifa na Dodoso?*
*14.5 Ninawezaje kuomba kuungana na familia?*

**Sehemu ya 15 Malazi Yako**

*15.1 Maelezo ya mapokezi/malezi*

**Kiambatisho - Maelezo ya Mawasiliano**

# Sehemu ya 1
# Ulinzi wa Kimataifa ni nini na ninawezaje kutuma maombi yangu?

## 1.1 Je, ulinzi wa kimataifa ni nini?

1.1.1 Kuna aina mbili za ulinzi wa kimataifa zinazoshughulikiwa na Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015 zinazoitwa hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala.

**Hadhi ya ukimbizi**

1.1.2 Ili utambuliwe kama *mkimbizi*, ni lazima uwe mtu ambaye ana hofu inayoaminika ya kuteswa kwa sababu za:

(i) umbari,
(ii) dini,
(iii) uraia,
(iv) maoni ya kisiasa au
(v) uanachama wa kundi maalum la jamii,

lazima uwe nje ya nchi yako ya uraia na huwezi au, kwa sababu ya hofu hiyo, hutaki kulindwa na nchi hiyo, au wewe ni mtu asiyekuwa na uraia, ambaye kwa sababu ya kuwa nje ya nchi yake ya makazi ya zamani kwa sababu zile zilizotajwa hapa juu, hawezi au, kwa sababu ya hofu hiyo, hataki kurejea nchi hiyo.

**Hali ya hifadhi mbadala**

1.1.3 Kama itaamuliwa kuwa wewe si mkimbizi, unaweza ukafaa *hifadhi mbadala kama kuna sababu thabiti za kuaminika kuwa uko kwenye hatari ya kweli ya kupitia madhara makubwa ikiwa utarejeshwa nchi yako ya asili/nchi yako ya makazi ya zamani.* Angalia **sehemu ya 2.5.1** kwa maelezo zaidi.

## 1.2 Ni nani anayeweza kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa?

1.2.1 Mtu ambaye ana umri wa miaka 18 na zaidi na ambaye yuko kwenye mipaka ya Nchi (Ayalandi) au aliye ndani ya Nchi (Ayalandi) anaweza kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa

(a) kwa niaba yake mwenyewe

(b) kwa niaba ya mtu mwingine ambaye ako chini ya umri wa miaka 18 ambaye anawajibika kumlea na kumlinda.

1.2.2 Hii inategemea maombi yanayorejelewa katika **aya ya 1.2.1**
(a) kupatikana kuwa unakubalika (**angalia aya ya 3.3**), au

(b) kama ni maombi ya kufuatilia, kukubalika kwa kibali cha Waziri (angalia **sehemu ya 3.4**).

Tafadhali angalia pia **sehemu ya 3.13** kuhusu watoto wanaokutegemea.

### 1.3 Je, kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa ni hatua nzuri ya kuchukua katika hali yangu binafsi?

1.3.1 Unastahili kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa ikiwa una hofu ya kurejea nchi yako ya asili/nchi ya makazi/uraia wako wa zamani.

1.3.2 Kama una sababu nyingine za kutafuta kusalia Nchini (Ayalandi) tafadhali rejelea tovuti ya www.inis.gov.ie kwa maelezo.

### 1.4 Ni wapi ninastahili kutuma maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?

1.4.1 Lazima utume maombi yako **wewe mwenyewe** kwa Waziri. Unastahili kufanya hivi haraka uwezavyo, aidha kwenye uwanja wa ndege au bandarini ukiwasili nchini Ayalandi au (baada ya kungia Nchini), kwa

**International Protection Office,**
**Irish Naturalisation and Immigration Service,**
**79-83 Lower Mount Street,**
**Dublin 2.**
**D02 ND99**

### 1.5 Ni nani atashughulikia maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?

1.5.1 Kwa kuomba ulinzi wa kimataifa, unaomba kuwa Waziri azingatie kama unafaa kutangazwa kuwa mkimbizi au kutangazwa kama anayefaa hifadhi mbadala.

1.5.2 Kama sehemu ya utaratibu wa kutuma ombi moja, maombi yako ya ulinzi wa kitaifa kwa kawaida yatachunguzwa na maafisa, wanaojulikana kama Maafisa wa Ulinzi wa Kimataifa katika Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa. Hii ni sehemu ya Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi, ambayo iko katika Idara ya Haki na Usawa. Watu wengine katika IPO wanaweza kuhusika katika mchakato huu.

### 1.6 Kibali cha kusalia ni nini na ninawezaje kutuma maombi yangu?

1.6.1 Kama IPO itapendekeza kwamba huna haki ya kupata hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala, Waziri atafikiria kama atakupa kibali cha kusalia Nchini (Ayalandi) kwa sababu nyingine (kwa mfano, kwa sababu ya familia yako au hali za kibinafsi). Kazi hii itatekelezwa katika Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa. Lazima uweke maelezo muhimu kwenye sehemu inayofaa ya Dodoso la Ulinzi wa Kimataifa. Lazima ujulishe pia IPO kuhusu mabadiliko yoyote katika hali yako ambayo yanaweza kuwa muhimu kwa uamuzi wa kukupa au kukunyima kibali cha kusalia.

Hii imeshughulikia kwa undani zaidi katika **Sehemu ya 13.**

### 1.7 Je, kuungana na Familia ni nini?

17.1 Kama utapewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala, unaweza kutuma maombi kwa Waziri, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kupewa, kibali kwa wanafamilia wengine wa familia yako kuingia na kuishi na wewe Nchini (Ayalandi). **Hii inahusu wanandoa, wapenzi wanaotambuliwa na serikali (ambapo ulikuwa umeolewa au katika uhusiano wa ndoa na mtu huyo wakati wa tarehe ya maombi yako ya ulinzi) watoto ambao hawajaolewa chini ya umri wa miaka 16 na, katika hali ambayo mtoto amepewa ulinzi, watoto na ndugu za waombaji ambao wako chini ya umri wa miaka 18.**

1.7.2 Waziri atachunguza maombi na, kama ameridhishwa kuwa mtu huyo ni mwanafamilia wako anayesimamiwa na mahitaji ya kuungana na familia, atampa mtu huyo kibali cha kusalia.

1.7.3 Huenda Waziri akakataa kutoa kibali kwa mwanafamilia kwa sababu kadhaa ikiwa ni pamoja na usalama wa umma, sera za umma au amri ya umma au ambapo mwanafamilia huyo anawezakuwa, au hakubaliki kuwa mkimbizi au mtu anayefaa hifadhi mbadala.

1.7.4 Ni muhimu kukumbuka kwamba wakati unapotuma maombi ya ulinzi wa kimataifa unahitajika kutoa maelezo yote ya wanafamilia ambao wanaweza kufaa kuungana na familia iwapo watapewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala na Waziri.

1.7.5 Kwa maelezo zaidi tafadhali angalia **Sehemu ya 14**.

## Sehemu ya 2
## Maneno Muhimu

### 2.1 Je, Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa ni nini (IPO)?

2.1.1 IPO ni ofisi katika Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi (INIS), inayowajibika kuchunguza na kuchakata maombi ya ulinzi wa kimataifa. Mkuu wa IPO ndiye Afisa Mkuu wa Ulinzi wa Kimataifa, ambaye anaongoza timu ya maafisa wa ulinzi wa kimataifa. Wahudumu wa IPO wataamua pia, kwa niaba ya Waziri, kama kibali cha kusalia Nchini (Ayalandi) kitatolewa au kwa sababu nyingine kama waombaji wasiofanikiwa watapata ulinzi wa kimataifa.

### 2.2 Je, Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa ni nini (IPAT)?

2.2.1 IPAT ni shirika huru la kisheria lililoanzishwa ili kuamua maombi ya rufaa ya ulinzi wa kimataifa na kazi nyingine za maombi ya rufaa iliyopewa na Sheria ya Ulinzi ya Kimataifa ya 2015 na sheria nyingine muhimu.

### 2.3 Waziri ni nani?

2.3.1 Waziri ni Waziri wa Haki na Usawa.

### 2.4 Je, ni nani anayechukuliwa kama mkimbizi?

2.4.1 Ili utambuliwe kama *mkimbizi*, ni lazima uwe mtu ambaye ana hofu inayoaminika ya kuteswa kwa sababu za

(i) umbari,
(ii) dini,
(iii) uraia,
(iv) maoni ya kisiasa au
(v) uanachama wa kundi maalum la jamii,

lazima uwe nje ya nchi yako ya uraia na huwezi au, kwa sababu ya hofu hiyo, hutaki kulindwa na nchi hiyo, au wewe ni mtu asiyekuwa na uraia, ambaye kwa sababu ya kuwa nje ya nchi yake ya makazi ya zamani kwa sababu zile zilizotajwa hapa juu, hawezi au, kwa sababu ya hofu hiyo, hataki kurejea nchi hiyo.

Kuna makundi mengine ya watu ambao hawakubaliwi kupata hadhi ya ukimbizi **(angalia sehemu ya 2.8)**.

### 2.5 Je, ni nani anayefaa hifadhi mbadala?

2.5.1 Hii ni hadhi ambayo inafanana na ile ya ukimbizi. Inapewa watu ambao hawafai kuwa wakimbizi lakini ambao IPO inawachukulia kuwa ni watu ambao wako katika hatari ya kupata madhara makubwa wakirejea nchi yao ya asili.

Ufafanuzi sahihi ni kuwa *mtu anayefaa hifadhi mbadala* ni mtu ambaye

(i) si raia wa Nchi Mwanachama wa Umoja wa Ulaya,

(ii) hafai kuwa mkimbizi,

(iii) kulingana na sababu thabiti ambayo inaaminika kuwa, akirejea nchi yake ya asili/nchi yake ya makazi ya zamani, anaweza kukabiliana na hatari ya madhara makubwa, na ambaye hawezi, au hataki, kulindwa na nchi hiyo; na

(iv) ambaye anakubaliwa kupata hifadhi mbadala kwa sababu fulani. Tafadhali angalia aya ya **2.8.2**.

## 2.6 Je, madhara makubwa ni nini?

2.6.1 *Madhara makubwa* humaanisha:

(i) hukumu ya kifo au kunyongwa,

(ii) mateso au unyama au udhalilishaji au adhabu ya mtu katika nchi yake ya asili/nchi ya makazi yake ya zamani, au

(iii) tishio kali na tishio la kibinafsi kwa maisha ya uraia au mtu kwa sababu ya ukatili wa kiholela katika hali za migogoro ya kimataifa au kujihami kindani.

## 2.7 Je, makatazo ya kurejeshwa nchi ya nyumbani ni nini?

2.7.1 Makatazo ya kurejeshwa nchi ya nyumbani humaanisha Waziri hatamfukuza au kumrejesha mtu kwenye mpaka ambao, kwa maoni ya Waziri,

(i) maisha au uhuru wa mtu huyo utatishiwa kwa sababu za umbari, dini, uraia, uanachama wa kundi fulani la kijamii au maoni ya kisiasa, au

(ii) kuna hatari kubwa kuwa mtu huyo anaweza kupewa adhabu ya kifo, kuteswa au kutendewa unyama au udhalilishaji au adhabu.

Lazima Waziri atii jukumu hili iwe mtu huyo amepewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala au la.

## 2.8 Je, ni nani haruhusiwi kupata ulinzi wa kimataifa?

2.8.1 Mtu haruhusiwi kuwa mkimbizi wakati:

(i) anapokea ulinzi au usaidizi kutoka kwa mashirika au mawakala wa Umoja wa Mataifa (kando na Tume ya Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa (UNHCR), kama vile Wakala Wa Kazi na Misaada wa Umoja wa Mataifa (UNRWA), na kwamba ulinzi au usaidizi haujakomeshwa.

(ii) ametambuliwa na mamlaka husika ya nchi ambayo amechukua makazi kama ana haki na majukumu ambayo yameambatishwa kwenye umiliki wa uraia wa nchi hiyo, au haki na majukumu kwa wale, au

(iii) kuna sababu kali za kuaminika kuwa:

a. ametekeleza uhalifu dhidi ya amani, uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya binadamu, kama ilivyofafanuliwa katika vyombo vya kimataifa vilivyoandaliwa kutoa matoleo kuhusiana na uhalifu kama huo,

b. ametekeleza uhalifu mkali usio wa kisiasa nje ya Nchi hii (Ayalandi) kabla ya kuwasili Nchini (Ayalandi), au

c. amepatikana na makosa ya kutenda kinyume na malengo na kanuni za Umoja wa Mataifa.

Tafadhali kumbuka kwamba kutoruhusiwa kwake kunatumika pia ambapo kuna sababu kali za kufikiria kwamba mtu huyo amechochea au amehusika katika kutekeleza uhalifu au vitendo vilivyorejelewa katika (iii).

2.8.2 Mtu haruhusiwi kupata hifadhi mbadala wakati kuna sababu kali za kufikiria kuwa:

(i) ametekeleza uhalifu dhidi ya amani, uhalifu wa kivita, uhalifu dhidi ya binadamu, kama ilivyofafanuliwa katika vyombo vya kimataifa vilivyoandaliwa kutoa matoleo kuhusiana na uhalifu kama huo,

(ii) ametekeleza uhalifu mkali,

(iii) amepatikana na makosa ya kutenda kinyume na malengo na kanuni za Umoja wa Mataifa, au

(iv) ni mtu hatari kwa jamii au usalama wa Nchi (Ayalandi).

Tafadhali kumbuka kwamba kutoruhusiwa kwake kunatumika pia ambapo kuna sababu kali za kufikiria kwamba mtu huyo amechochea au amehusika katika kutekeleza uhalifu au vitendo vilivyorejelewa katika (i) – (iv).

2.8.3 Mtu haruhusiwi kupata hifadhi mbadala kama, kabla ya kuwasili kwake Nchini (Ayalandi), ametekeleza uhalifu ambao haujarejelewa katika **aya ya 2.8.2** ambapo, kama ulitekelezwa Nchini (Ayalandi), unaweza kuadhibiwa kwa kifungo na kama alitoroka nchi yake ya asili/nchi ya makazi yake ya awali ili kuepuka vikwazo vinavyotokana na uhalifu huo.

## 2.9 EURODAC ni nini?

EURODAC ni mfumo wa kielektroniki wa kubadilisha na kulinganisha alama za vidole kati ya Nchi Husika kwa utekelezaji sahihi wa Kanuni za EU Dublin. Tafadhali soma sehemu ya 10 kwa maelezo kuhusu Kanuni za EU Dublin.

## 2.10 Je, Eneo la Kawaida la Usafiri ni nini?

2.10.1 Eneo la Kawaida la Usafiri (CTA) linajumuisha Ayalandi, Uingereza, Visawa vya Channel na Kisiwa cha Isle of Man.

## Sehemu ya 3
## Mchakato wa Ulinzi wa Kimataifa

### 3.1 Ninastahili kutarajia nini wakati ninapoomba ulinzi wa kimataifa?

3.1.1 Wakati unapoomba ulinzi wa kimataifa unastahili kutarajia kuwa:

(i) Utatendewa kwa heshima, uadilifu na kwa haki haijalishi umri wako, ulemavu, uraia, jamii, umbari, jinsia, mapendeleo ya kimapenzi, dini au imani.

(ii) IPO inatambua kuwa mchakato huu unaweza kuwa si wa kawaida kwako na kuwa unaweza kuwa umepitia mambo ya kiwewe, na huenda ukapata kuwa ni vigumu kufichua maelezo nyeti kukuhusu.

(iii) Ili hali zako za kibinafsi ziweze kuzingatiwa kikamilifu wakati wa kuzingatia maombi yako, IPO inakutaka uhisi salama kushiriki maelezo yoyote nyeti, kwa mfano, kuhusu kubakwa, mateso, unyama wowote, au mapendeleo yako ya kimapenzi, ambayo ni muhimu kwa maombi yako. Maelezo yote yaliyotolewa kuhusiana na maombi yako yatashughulikiwa kwa siri kulingana na sheria na hayatafichuliwa kwa mamlaka ya nchi yako ya nyumbani au kwa wawakilishi wa nchi yako nchini Ayalandi.

(iv) Ikiwa ni rahisi kwako kuongea na mwanaume au mwanamke kuhusu masaibu yako, IPO itakubali maombi kama hayo, ikiwezekana.

(v) Utaulizwa kama uko sawa kuongea na IPO kwa Kiingereza au kama utahitaji mkalimani. Una haki, ikiwa inafaa na inawezekana, ya kupewa mkalimani ili kuhakikisha mawasiliano yanayostahili.

### 3.2 Ni hatua zipi za kwanza katika mchakato huu wa maombi?

3.2.1 Ni muhimu kukumbuka kwamba kabla ya kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa ni lazima kwamba ukamilisha mahojiano ya mwanzo ambayo yatahusisha kuzingatia kama maombi yako yanaweza kukubalika au la au kama yanaweza kukubaliwa na IPO.

### 3.3 Ukubalifu wa maombi yangu utabainishwa aje?

3.3.1 Kabla utume maombi ya ulinzi wa kimataifa ni lazima, kama sehemu ya mahojiano ya mwanzo, uridhishe ofisi ya ulinzi wa kimataifa kuwa maombi yako yanaweza kukubalika.

3.3.2 Maombi yako hayatakubalika (na hutakuwa na haki ya kuomba ulinzi) kama:

(i) Nchini nyingine mwanachama wa EU imekupa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala na/au

(ii) nchi, tofauti na nchi mwanachama wa EU

a. imekutambua kama mkimbizi na unaweza bado kutumia ulinzi huo, au

b. una ulinzi wa kutosha wa nchi hiyo, pamoja na faida ya kanuni ya kutoweza kurejeshwa nchi ya nyumbani na unaweza kuchukuliwa tena katika nchi hiyo.

3.3.3 Afisa wa ulinzi wa kimataifa atapendekeza kuhusu ukubalifu wa maombi yako kufuatia mahojiano ya mwanzo.

3.3.4 Iwapo utapokea mapendekezo kutoka kwa afisa wa ulinzi wa kimataifa kuwa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa hayawezi kukubaliwa, utapokea taarifa iliyoandikwa na sababu.

3.3.5 Una haki ya kukata rufaa pendekezo hilo kwa IPAT katika kipindi husika cha sheria. Maelezo zaidi kuhusu kukata rufaa yanaweza kupatikana katika **sehemu ya 5. Uamuzi wa IPAT utafanywa bila usikilizaji wa kusimulia.**

3.3.6 Kama afisa wa ulinzi wa kimataifa atapendekeza kuwa maombi yako hayawezi kukubaliwa, na pendekezo hilo lithibitishwe na IPAT, lazima Waziri amue kuwa maombi yako hayakubaliwi.

3.3.7 Kama maombi yatapatikana kuwa hayakubaliwi, aidha na IPO au IPAT, uamuzi huo utakubaliwa na Waziri wa uchunguzi na kuamuliwa na IPO.

## 3.4 Ikiwa tayari nimepokea uamuzi wa maombi ya awali ya ulinzi wa kimataifa, ninaweza kutuma maombi mengine (maombi ya kufuatia)?

3.4.1 Mtu hawezi kutuma maombi ya pili au mengine (*maombi ya kufuatia*) ya ulinzi wa kimataifa bila kibali cha Waziri.

3.4.2 Maombi ya kibali cha Waziri cha kutuma maombi ya kufuatia ya ulinzi wa kimataifa yanastahili kufanywa kwa kumwandikia Waziri na yatazingatiwa na afisa wa ulinzi wa kimataifa.

3.4.3 Ili uweze kuwa na haki ya kutuma maombi ya kufuatia, lazima utimize masharti yafuatayo:

(i) Tangu uamuzi wa awali wa maombi ya ulinzi wa kimataifa, mambo au matokeo mapya yameibuka au yamewasilishwa na wewe ambapo yanafanya uwe na uwezekano zaidi kuwa utafaa ulinzi wa kimataifa,

na

hukuweza kuwasilisha mambo au matokeo haya kwa madhumuni ya maombi yako ya awali kwa sababu ya makosa yao wenyewe,

au

(ii) Kama maombi ya awali yaliondolewa au kuonekana kuwa yameondolewa, haungeweza kufuatilia maombi yako ya awali wakati huo wa kuondolewa au kuonekana kuwa yameondolewa, na haikuwa sababu yako.

3.4.4 Kama afisa wa ulinzi wa kimataifa atapendekeza kuwa Waziri anastahili kukupa kibali cha kutuma maombi ya kufuatia, Waziri huyo atakupa kibali hicho na kisha unaweza kutuma maombi yako.

Kama afisa wa ulinzi wa kimataifa atapendekeza kuwa Waziri hastahili kukupa kibali chake cha kutuma maombi yako ya kufuatia, utapokea taarifa iliyoandikwa na sababu.

3.4.5 Una haki ya kukata rufaa ya pendekezo hilo la mwisho kwa IPAT katika kipindi husika cha sheria. Maelezo zaidi kuhusu kukata rufaa yanaweza kupatikana katika **sehemu ya 5. Uamuzi wa IPAT utafanywa bila usikilizaji wa kusimulia.** Ukikosa kukata rufaa, Waziri atakataa kukupa kibali cha kutuma maombi ya kufuatia.

3.4.6 Ukifanikiwa katika maombi yako ya rufaa, Waziri atakupa kibali cha kutuma maombi ya kufuatia. 3.4.6 Ukikosa kufanikiwa katika maombi yako ya rufaa kwa IPAT, Waziri atakataa kukupa kibali cha kutuma maombi ya kufuatia.

## 3.5 Je, mahojiano ya mwanzo ni nini?

3.5.1 Wakati unakamilisha mahojiano ya mwanzo, utaulizwa, kati ya mambo mengine, baadhi ya maswali yanayohusiana na

(i) kama ungependa kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa na, kama ni hivyo, sababu za kawaida za maombi yako,
(ii) utambulisho wako,
(iii) uraia wako,
(iv) nchi yako ya asili/nchi ya makazi yako ya zamani,
(v) njia mbayo ulisafiri ukija Nchini (Ayalandi), mbinu za usafiri zilizotumika na maelezo ya mtu yeyote aliyekusaidia kusafiri Ayalandi,
(vi) sababu za kuja Ayalandi,
(vii) msingi wa kisheria wa kuingia au uwepo wako Nchini (Ayalandi).

3.5.2 Utaulizwa pia baadhi ya maswali ili kubainisha kama unaweza kukubaliwa katika mchakato wa ulinzi wa kimataifa (**angalia sehemu ya 3.3. na 3.4**).

3.5.3 Mahojiano haya ya mwanzo yatatekelezwa kwa usaidizi wa mkalimani ikiwa inafaa na inawezekana.

3.5.4 Taarifa ya mahojiano haya ya mwanzo itawekwa na afisa anayeitekeleza. Utasomewa na utakuwa na nafasi ya kusahihisha taarifa hiyo ikiwa utahitajika kufanya hivyo. Utaulizwa utie saini azimio la kuthibitisha kuwa maelezo uliyoyatoa ni sahihi na hata pia masahihisho au mabadiliko yoyote uliyoyafanya. Ni muhimu sana usome azimio hili kwa makini ili uhakikishe kuwa linajumuisha maelezo yote muhimu ambayo umeyatoa. Ni wajibu wako kuhakikisha kuwa wakati wa mahojiano hujatajwa vibaya au kueleweka vibaya. Kisha utapewa nakala ya taarifa hii ya mahojiano.

3.5.5 Kufuatia mahojiano haya ya mwanzo, kama maombi yako yatapatikana kuwa yanakubalika, utaruhusiwa kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa kwa kujaza fomu ya maombi.

## 3.6 Je, alama zangu za vidole na maelezo mengine ya biometriki yatachukuliwa?

3.6.1 IPO watachukua maelezo yako ya biometriki. Hii inahusisha kuchukua alama zako za vidole na picha yako. Hii ni kwa madhumuni ya kujua utambulisho wako na kukagua kama ulikuwa umatuma maombi ya ulinzi wa kimataifa hapo awali au la katika Nchi Husika katika Kanuni za EU Dublin (**angalia sehemu ya 10**). Maelezo haya yatalinganishwa na hifadhidata nyingine (pamoja na EURODAC na visas) ili kuhakikisha kuwa Ayalandi ndio nchi inayowajibika katika kuchunguza maombi yako.
Alama za vidole zitachukuliwa kutoka kwa mtu chini ya umri wa miaka 14 katika uwepo wa wazazi au mtu mzima mlezi, kama inawezekana, mtu aliyeteuliwa na TUSLA - Shirika la Watoto na Familia ili kutuma maombi na kumwakilisha mwombaji wakati wa mchakato huu.

## 3.7 Je, nitapokea maelezo yaliyoandikwa kuhusu mchakato wa ulinzi wa kimataifa?

3.7.1 Pamoja na kijitabu hiki utapewa Maombi ya Dodoso la Ulinzi wa Kimataifa ambayo ni lazima ikamilishe na irejeshwe kwa IPO. Lazima urejeshe dodoso hili kabla ya tarehe na saa iliyobainishwa na IPO.

**Ukishindwa kurejesha dodoso lako kabla ya tarehe iliyobainishwa, huenda ukachukuliwa kuwa umeshindwa katika jukumu lako la kushirikiana katika uchunguzi wa maombi yako. Katika suala hili, tafadhali rejelea sehemu ya 4.4 na sehemu ya 8.2.**

3.7.2 Inapendekezwa kwamba upate ushauri wa kisheria kabla ya kukamilisha dodoso lako.

## 3.8 Je, ninastahili kubeba nini wakati ninatuma maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?

3.8.1 Unastahili kubeba hati yoyote unayomiliki kwa IPO wakati unatuma maombi yako. Hii ni pamoja na

- **Pasipoti** - hii ni pamoja na pasipoti yako, na pasipoti ya mpenzi wako na/au mtu yeyote anayekutegemea nchini Ayalandi (kama inatumika). Hii ni ya kusaidia IPO kujua umri, utambulisho na uraia wako. Kama ulitumia pasipoti bandia kwa safari yako kuja Ayalandi unastahili pia kuibeba.

- **Hati yoyote ya kusafiri** - hii ni pamoja na tiketi za safari na pasi za kuabiri, hata kama hazikutolewa kwa kutumia jina lililo kwenye pasipoti au hati ya utambulisho wa taifa iliyotumiwa kusafiri.

- **Hati nyingine** - hii ni pamoja na kadi za utambulisho, vyeti vya kuzaliwa/ndoa/shule, kadi za uanachama na hati nyingine muhimu kwa madai yako.

3.8.2 Unastahili kupatia IPO **hati zote zinazopatikana** za kuunga mkono maombi yako **haraka iwezekanavyo.** Unastahili kuzibeba ukienda kwa IPO au kama huwezi kufanya hivi wakati unatuma maombi yako ya ulinzi wa kimataifa, unastahili kuziwasilisha haraka iwezekanavyo na mapema au katika mahojiano yako ya ulinzi wa kimataifa. Kama huwezi kutimiza mahitaji haya, unastahili kupatia IPO hati zozote za ziada katika muda ambao utapewa wakati wa mahojiano yako ya ulinzi wa kimataifa.

3.8.3 Kulingana na hali husika, kushindwa kupeana hati hizi kunaweza kuchukuliwa kuwa **umeshindwa katika jukumu lako la kushirikiana** na mchakato wa ulinzi wa kimataifa. Tafadhali rejelea **sehemu ya 4.4 na sehemu ya 8.2.**

## 3.9 Je, Cheti cha Makazi ya Muda (TRC) ni nini na nitakipokea lini?

3.9.1 Wakati unapotuma maombi ya ulinzi wa kimataifa na maombi hayo yapatikane kuwa hayakubaliki, kama sehemu ya mchakato wa kwanza wa usajili, utapokea Cheti cha Makazi ya Muda (TRC). TRC ni ushahidi kwamba umewasilisha maombi ya ulinzi nchini Ayalandi.

3.9.2 TRC **sio** kitambulisho na wala sio thibitisho la utambulisho wako lakini itakuwa na maelezo ya kibinafsi uliyotoa kwa IPO, ikiwa ni pamoja na jina lako, tarehe ya kuzaliwa na uraia wako, na hata pia picha yako.

3.9.3 TRC, ambayo inaweza kubadilishwa upya, hubakia kuwa mali ya Waziri na nilazima uiwasilishe ukiombwa ufanye hivyo na Waziri. TRC yako itakuwa batili wakati kibali chako cha kuingia na kuishi Nchini (Ayalandi) kama mwombaji wa ulinzi, kitakapokoma kuwa halali.

3.9.4 Tafadhali hakikisha kuwa umesasisha TRC yako kwa kuwa huonyesha una kibali cha kuwa Nchini (Ayalandi) kwa madhumuni ya maombi yako ya ulinzi wa kimataifa.

### 3.10 Je, na nikiwa mlemavu au niwe na mahitaji maalum?

3.10.1 Tafadhali elezea IPO haraka uwezavyo kuhusu mahitaji yoyote maalum ya mahojiano yako. Unastahili pia kufahamisha IPO kuhusu mahitaji yoyote maalum siku hiyo ya kutuma maombi yako. Ikiwezekana, IPO watajaribu kushughulikia mahitaji yoyote wanayoweza ambayo utatufahamisha.

### 3.11 Je, ninaweza kuomba ulinzi wa kimataifa nikiwa mfungwa au kizuizini?

3.11.1 Unaweza kuomba ulinzi wa kimataifa hata kama wewe ni mfungwa au uko kizuizini nchini (Ayalandi). Unaweza tu kuomba ulinzi kupitia Gavana wa taasisi ambayo umefungwa. Unastahili kujulisha Ofisi ya Serikali mara moja iwapo ungependa kuomba ulinzi. Kisha Ofisi ya Serikali itafanya mipango kabambe na IPO ya kuchakata maombi yako.

3.11.2 IPO itaipa kipaumbele uchunguzi na uamuzi wa maombi kutoka kwa mtu aliyefungwa.

### 3.12 Ni hali gani ambazo mwombaji wa ulinzi wa kimataifa anaweza kufungwa?

3.12.1 Afisa wa uhamiaji au afisa wa Garda Síochána anaweza kumkamata mwombaji bila kibali kama anashuku kuwa mwombaji:

(i) ni tishio kwa usalama wa umma au utulivu wa umma Nchini (Ayalandi),

(ii) ametekeleza uhalifu mkali ambao si wa kisiasa nje ya Nchini (Ayalandi).

(iii) hajafanya juhudi zozote za kuonyesha utambulisho wake,

(iv) anakusudia kuondoka Nchini (Ayalandi) bila mamlaka ya kisheria ya kuingia nchi nyingine,

(v) amefanya au anakusudia kutenda kwa njia ambayo itadhoofisha -

- mfumo wa kuwapa watu ulinzi wa kimataifa Nchini (Ayalandi), au
- mipango yoyote inayohusiana na Eneo la Kawaida la Usafiri (angalia **sehemu ya 2.10**), au

(vi) bila sababu inayoeleweka -

- ameharibu kitambulisho au hati yake ya kusafiri, au
- anamiliki au amekuwa akimiliki hati ghushi, iliyobadilishwa ya utambulisho.

3.12.2 Ukikamatwa kwa sababu yoyote hapa juu, unaweza kupelekwa mahali palipotengwa pa kizuizini. Mtu ambaye amefungwa atapelekwa mbele ya Mahakama ya Wilaya haraka kama iwezekanavyo, ambayo inaweza kumfunga mtu huyo kwa kipindi cha hadi siku 21, au kumwachilia kwa masharti. Kipindi cha kufungwa kinaweza kubadilishwa mara kwa mara hadi siku 21 kulingana na uamuzi wa maombi ya ulinzi wa kimataifa. Mtu aliyefungwa chini ya matokeo haya ana haki ya kushauriana na wakili, na kupokea usaidizi wa mkalimani kwa lengo la ushauri wa mwakilishi wa kisheria na kutokea mahakamani.

## 3.13 Je, ni nini hufanyika ikiwa nina watu wanaonitegemea chini ya umri wa miaka 18?

3.13.1 Bora si raia wa Ayalandi, mtoto anayekutegemea chini ya umri wa miaka 18 atachukuliwa kuwa amehusishwa katika maombi yako. Dhana hii inatumika iwe mtoto alikuwepo Nchini (Ayalandi) au wakati wa kutuma maombi yako.

3.13.2 Kwa hivyo, kama utatuma maombi ya ulinzi wa kimataifa, utachukuliwa kuwa umetuma maombi kwa niaba ya mtoto wako anayekutegemea ambaye si raia wa Ayalandi na

(a) wakati wa kutuma maombi haya, yuko Nchini (Ayalandi) na yuko chini ya umri wa miaka 18,

(b) amezaliwa Nchini (Ayalandi) ukiwa mwombaji,

(c) ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 na ameingia Nchini (Ayalandi) ukiwa mwombaji.

3.12.3 Kama unaomba ulinzi wa kimataifa na una watoto wanaokutegemea, lazima uje nao kwa IPO wakati unapotuma maombi yako.

3.13.4 **Muhimu: Kama mtoto wako amezaliwa baada ya kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa, au mtu yeyote anayekutegemea amewasili Nchini (Ayalandi) baada ya maombi yako kutumwa, lazima ulete mtoto/watoto hao kwa IPO mara moja.**

## 3.14 Je, ni wapi ninaweza kupata ushauri wa kisheria?

3.14.1 Una haki ya kushauriana na mwakilishi wa kisheria kuhusu kutuma maombi yako ya ulinzi wa kimataifa. Unaweza kutumia huduma za Bodi ya Usaidizi wa Kisheria (LAB) ambayo

(i) itakupa usaidizi na ushauri wa kisheria wa kuunga mkono maombi yako.

(ii) Itakushauri kuhusu kukamilisha Dodoso lako la Ulinzi wa Kimataifa pamoja na sababu zozote ambazo ungependa kusema kwa lengo la kumwomba Waziri kukupa kibali cha kusalia Nchini (Ayalandi).

(iii) Itakusaidia kukuandaa kwa mahojiano yako ya ulinzi wa kimataifa na uwakilishi wowote uliondikwa kwa Waziri.

(iv) katika hali ya mapendekezo ya kupinga kuhusu maombi yako, itakupa uwakilishi katika maombi yoyote ya rufaa ambayo unaweza kuyapeleka kwa Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa (IPAT).

3.14.2 Maelezo ya mawasiliano ya LAB yamewekwa katika **Kiambatisho** kwenye hati hii.

3.14.3 Kama hutaki kutumia huduma za LAB unaweza kutafuta huduma za mwakilishi binafsi wa kisheria kwa gharama zako mwenyewe. Ukichagua kushauriana na mwakilishi binafsi wa kisheria lazima uhakikishe kuwa amesajiliwa kama mwanasheria au wakili Nchini (Ayalandi).

### 3.15 Je, ninaweza kuondoa maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?

3.15.1 Kwa ujumla unaweza kuondoa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa wakati wowote ule kabla ya taarifa kuhusu maombi yako kuandaliwa na afisa wa ulinzi wa kimataifa. Unaweza kufanya hivi kwa kutuma taarifa ya kuondolewa kwa maombi yako kwa IPO. Taarifa hii inastahili kujumuisha anwani yako mpya, nambari yako ya rejeleo na saini yako. Kama una watoto wanaokutegemea katika maombi yako, unastahili kujumuisha maelezo yao kwenye ilani ya kuondoa.

3.15.2 Athari ya kuondoa maombi yako itakuwa kuwa maombi kwa IPAT hayatapatikana na Waziri atakataa kukupa hadhi ya ukimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala. Hata hivyo, tafadhali kumbuka kuwa Waziri hataendelea kuzingatia kama unastahili kupewa kibali cha kusalia kwa sababu nyingine. Isipokuwa uwe na sababu nyingine ya kusalia Nchini (Ayalandi), una uwezekano wa kupata amri ya kufukuzwa nchini.

3.15.3 Kabla ya kuondoa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa unastahili kutafuta ushauri wa kisheria ili uhakikishe kuwa unafahamu vikamilifu matokeo ya uamuzi wako.

## Sehemu ya 4
## Mahojiano na Uchunguzi

### 4. 1 Je, ni nini ninastahili kutarajia katika mahojiano yangu ya ulinzi wa kimataifa?

4.1.1 Utapewa maelezo kuhusu tarehe, saa na mahali pa mahojiano yako ya ulinzi wa kimataifa kwa **barua iliyoandikwa na IPO**. Mahojiano yako yatatekelezwa faraghani. Kama umeomba afisa wa kuhoji, au mkalimani mwanaume au mwanamke, IPO itapanga kama itawezekana.

4.1.2 Mahojiano yako ni nafasi yako ya kuongea na IPO uso kwa uso na kutoa maelezo yako kamili kuhusu ni kwanini uliondoka nchi ya asili/nchi ya makazi yako ya awali na ni kwanini unahofia kurejea huko. Ni muhimu kwamba uhudhurie mahojiano, ambayo tutayafanya yaweze kukutuliza kama iwezekanavyo. Ni muhimu sana utoe maelezo yako kamili ya yale yaliyokufanyikia kwa njia ya kweli na ni nani unayemwogopa, kama utarejea nchi yako ya asili/nchi ya makazi yako ya awali.

4.1.3 Tutakuhoji kwa lugha ambayo unaweza kuelewa na ambayo unaweza kuwasiliana nayo. Taarifa iliyoandikwa ya mahojiano itatengenezwa na afisa wa ulinzi wa kimataifa na itasomwa kwako mara kwa mara ili uweze kufanya marekebisho yoyote au kujumuisha maelezo zaidi. Utaulizwa utie saini kila karatasi ya taarifa ya mahojiano ili uthibitishe kuwa maelezo uliyoyatoa ni sahihi.

4.1.4 Ni muhimu sana utoe ushahidi wowote au maelezo ambayo unayo ili kuunga mkono maelezo yako wakati wa mahojiano yako (au mapema kama inawezekana), Kama una ushahidi zaidi ambao ungependa kuuwasilisha baada ya mahojiano, unastahili kufanya hivyo katika kipindi cha muda uliowekwa na IPO.

4.1.5 Tutazingatia maelezo yoyote maalum yanayohusiana na jinsia na mazingira yoyote magumu ambayo utayataja katika maombi yako au wakati wa mchakato wa uchunguzi.

4.1.6 **Hutaulizwa maswali yanayohusiana moja kwa moja na kibali cha kusalia katika mahojiano yako ya ulinzi**. **Mahojiano haya yatelenga maombi yako ya ulinzi.** Hata hivyo, kama masuala kama hayo yataibuka (kwa mfano, hali za familia yako), yataandikwa na afisa wa ulinzi wa kimataifa. Kama IPO itapendekeza kuwa hustahili kupewa ulinzi wa kimataifa, itazingatiwa kuwa unastahili kupewa kibali cha kubakia kwa sababu nyingine, na maelezo yoyote muhimu yaliyotoewa wakati wa mchakato wa maombi yatazingatiwa wakati huo.

**4.2 Je, ninaweza kumleta mtu yeyote kwa mahojiano yangu ya ulinzi wa kimataifa ili kunisaidia?**

4.2.1 Mahojiano yako yatatekelezwa faraghani. Mwakilishi wako wa kisheria anaweza kuhudhuria mahojiano hayo. Kama unapokea ushauri wa kisheria kutoka kwa Bodi ya Usaidizi wa Kisheria, unastahili kuwasiliana na mwakilishi wako wa kisheria kama wataweza kuhudhuria au la. Kwa ujumla, hakuna mtu mwingine ataweza kuhudhuria, isipokuwa uwe chini ya umri wa miaka 18 ambapo mlezi wako au mwakilishi kutoka TUSLA - Shirika la Watoto na Familia lazima ahudhurie.

4.2.2 Mtu anayekuzindikisha hataweza kujibu maswali yoyote kwa niaba yako.

4.2.3 Kama ungependa kumleta mwakilishi wa kisheria, ataruhusiwa kuangalia mahojiano. Mwakilishi wako wa kisheria atapewa nafasi mwanzo na mwisho wa mahojiano kutoa maoni yoyote ambayo anaona ni ya maana. Hataweza kujibu maswali yoyote kwa niaba yako.

**4.3 Na ikiwa siwezi kuhudhuria mahojiano au nishindwe kuhudhuria mahojiano yangu?**

4.3.1 Kwa sababu una jukumu la kushirikiana na mchakato huu wa uchunguzi, mahojiano yanaweza kuahirishwa tu kwa sababu za afya mbaya au sababu nyingine **zinazoruhusiwa**. Unastahili kufahamisha IPO **haraka iwezekanavyo** kama unafikiria una tatizo la kuja kwenye mahojiano yako. Unatarajiwa kutoa ushahidi wa kimatibabu kuhusu magonjwa yoyote kutoka kwa daktari wako (Daktari au mshauri) kwa IPO mapema kabla ya mahojiano.

4.3.2 Ukikosa kuhudhuria mahojiano ya kibinafsi tarehe na saa ambayo iliwekwa na ukose, ndani ya siku 3 za kazi kuanzia tarehe hiyo, kupatia IPO sababu inayoeleweka, IPO itaendelea kuchunguza maombi yako kwa msingi wa maelezo uliyowasilisha hadi wakati huo wa mchakato wa ulinzi. Kwa maneno mengine, utapoteza nafasi ya kuelezea masuala wakati wa mahojiano na maombi yatachunguzwa kulingana na dodoso na hati zozote ambazo umewasilisha kabla ya muda uliowekwa wa mahojiano.

**4.4 Je, nina jukumu la kushirikiana na mchakato wa maombi na matokeo yake ni gani nikishindwa kufanya hivyo?**

4.4.1 Ni wajibu wako kushirikiana na uchunguzi wa maombi ya ulinzi wa kimataifa.

4.4.2 Jukumu lako la kushirikiana ni pana na linajumuisha hitaji

(i) la kuwa mkweli na kuwasilisha haraka iwezekanavyo maelezo yote yanayohitajika ili kuthibitisha maombi yako (hii ni pamoja na taarifa na hati ambazo unazo kuhusiana na vipengee muhimu vya maombi yako), na

(ii) kushirikiana katika uchunguzi wa maombi yako katika kuamua maombi yoyote ya rufaa.

4.4.3 Unastahili pia kutii majukumu yale yote mengine katika Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015. Katika suala hili, tafadhali angalia **sehemu ya 8.**

4.4.4 Kama Waziri anafikiria

(i) kuwa unashindwa na jukumu lako la kushirikiana katika uchunguzi wa maombi yako, au

(ii) kuwa umekiuka majukumu yako ya kutoondoka au jaribio la kuondoka Nchini (Ayalandi) bila kibali cha Waziri, au

(iii) kuwa umekiuka majukumu yako ya kumfahamisha Waziri kuhusu anwani yako na mabadiliko yoyote ya anwani haraka iwezekanavyo, au

(iv) kuwa umekiuka majukumu yako ya kutii ilani ambayo ilikuhitaji:

- uishi na usalie katika wilaya au mahali fulani Nchini (Ayalandi)

  na

- kuripoti mara kwa mara kwa afisa wa uhamiaji, au katika kituo maalum cha Garda Síochána,

Waziri atakuarifu kwa kukuandikia maoni yake na kukualika, ndani ya siku 10 za kazi, umpatie maoni yako katika majibu yako. Utaulizwa uthibitishe kuwa unataka kuendelea na maombi yako na utakumbushwa kuhusu jukumu lako la kushirikiana.

4.4.5 Kama

(a) hutajibu,

au kufuatia kuzingatia majibu yako,

(b) Waziri aamue kuwa haushirikiani na mchakato wa ulinzi.

maombi yako yatachunguzwa kwa msingi wa maelezo uliyowasilisha kabla ya wakati huo.

## 4.5 Je, mchakato mkuu wa uchunguzi ni upi, pamoja na mahojiano ya kibinafsi?

4.5.1 IPO itachunguza maombi yako ya ulinzi wa kimataifa ili kujua::

- kwanza, kama unastahili hadhi ya ukimbizi au la, na kama ni la,
- kama una haki ya hifadhi mbadala au la.

4.5.2 Mchakato huu kwa kawaida uhitaji

- mahojiano ya kibinafsi,
- uchunguzi wa maombi yako pamoja na maelezo yaliyowasilishwa na wewe kwa kuandika au katika mahojiano na
- maandalizi ya taarifa kuhusu matokeo ya uchunguzi. Ripoti hii itajumuisha matokeo na mapendekezo ya kama unastahili au hustahili fomu ya ulinzi wa kimataifa.

**Mahojiano ya Kibinafsi**

4.5.3 Lengo la mahojiano ya kibinafsi ni kujua maelezo kamili ya madai ya ulinzi wa kimataifa. Wanandoa/wapenzi kwa kawaida uhojiwa kando.

4.5.4 Katika mahojiano, unastahili

(i) kufafanua waziwazi na kwa ufupi ni kwanini unatafuta ulinzi wa kimataifa,

(ii) kufafanua waziwazi na kwa ufupi ni kwanini unatafuta ulinzi wa kimataifa wa wanaokutegemea, kama wako,

(iii) kutoa maelezo, hati na taarifa zote ambazo ni muhimu kwa hali zako maalum na kwa wanaokutegemea na hasa, maelezo kuhusu ni kwa nini wewe na wanaokutegemea hawawezi kurejea nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani.

4.5.5 Ni wajibu wako kushirikiana kikamilifu na kuwa mkweli kabisa. Kushindwa kufanya hivi kunaweza kuathiri kuaminika kwako **na husababisha kuonekana kuwa hushirikiani katika uchunguzi wa maombi yako** (angalia **aya ya 4.4.4 na 4.4.5** hapa juu).

4.5.6 Mhoji anayetekeleza mahojiano, akifikiria inafaa, anaweza kuwahoji wanaokutegemea waliojumuishwa katika maombi yako.

4.5.7 Ili kuhakikisha mawasiliano yanayofaa mahojiano yatatekelezwa kwa usaidizi wa mkalimani, ikiwa atahitajika na anapatikana.

4.5.8 Mkalimani ana jukumu la kuheshimu hali ya usiri ya mahojiano, na haruhusiwi kufichua, kujadili, kutumia au kumpatia mtu yeyote maelezo yaliyokusanywa wakati wa kufanya kazi zake.

4.5.9 Utahojiwa na mhoji ambaye amepokea mafunzo ya kuhoji watu wanaotafuta ulinzi wa kimataifa na atakuwa na maelezo ya kina yanayopatikana kuhusu nchi yako ya asili/nchi ya makazi yako ya zamani.

4.5.10 Taarifa iliyoandikwa/kuchapishwa ya mahojiano itawekwa na mhoji. Utakuwa na nafasi ya kupitia taarifa hiyo na utaulizwa utie saini kila ukurasa ili uthibitishe kuwa ni maelezo sahihi ya mahojiano yako. **Kama unaamini kuwa kitu chochote kilichoandikwa au kuchapishwa katika maelezo haya si sahihi, unastahili kufahamisha mhoji moja kwa moja, na utapewa nafasi ya kuelezea wakati wa mahojiano.**

4.5.11 Unaweza kuwakilisha kwa kuandika kwa IPO kuhusu suala lolote linalohusika na uchunguzi wake wa maombi yako. Mtu mwingine yeyote anayehusika na maombi yako anaweza pia kufanya hivyo, hata pia UNCHR. Inapendekezwa kwamba uwakilishi kama huo ufanywe kabla ya mahojiano. IPO itazingatia uwakilishi wote kama huo uliyofanywa kabla au wakati wa mahojiano na wewe na inaweza pia kuzingatia taarifa iliyofanywa baada ya mahojiano bora iwe uliwasilisha kabla ya ripoti kukamilishwa kuhusiana na maombi.

4.5.12 Huenda mahojiano ya kibinafsi yakatekelezwa ambapo afisa wa ulinzi wa kimataifa ana maoni ya

(i) ushahidi unaopatikana unaashirikia kuwa mwombaji ni mtu anayestahili kupewa hadhi ya ukimbizi;

(ii) mwombaji, ambaye yuko chini ya miaka 18, ana umri mdogo na si mtu mzima kwa hivyo mahojiano hayatasaidia katika uchunguzi, au

(iii) mwombaji hafaii au hawezi kuhojiwa kwa sababu ambazo zinaendelea na ambazo haziwezi kuzidhibiti.

**Uchunguzi wa maombi yako na maandalizi ya mapendekezo**

### 4.6 Je, ni nini hufanyika baada ya mahojiano yangu?

4.6.1 IPO itazingatia maelezo yote muhimu yanayohusiana na maombi yako ya ulinzi wa kimataifa na kuandaa mapendekezo kulingana na hii.

## 4.7 Je, ni matokeo gani yanayowezekana ya maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa?

4.7.1 Afisa wa ulinzi wa kimataifa atakupa taarifa iliyoandikwa ya mapendekezo kuhusu maombi yako ya ulinzi wa kimataifa. Mapendekezo yatakuwa moja kati ya yafutayo:

(i) kuwa unastahili kupewa hadhi ya ukimbizi,

(ii) kuwa haupaswi kupewa hadhi ya ukimbizi lakini unastahili kupewa hifadhi mbadala, au

(iii) kuwa hustahili kupewa hadhi ya ukimbizi wala ya hifadhi mbadala.

4.7.2 Katika hali ambazo inapendekezwa usipewe hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala, taarifa ya ulinzi wa kimataifa inaweza pia kujumuisha matokeo yafuatayo:

(i) kuwa maombi yako yameibua masuala ambayo si muhimu au si ya maana kwako kustahili ulinzi wa kimataifa,

(ii) kuwa umetoa maelezo yasiyolingana, yanayopingana, si yamkini au yasiyotosha ambayo yanafanya madai yako ya kufaa ulinzi wa kimataifa yasiwezi kuridhisha.

(iii) kuwa umeshindwa bila sababu ya kuaminika kutuma maombi yako kwa wakati unaofaa na ulikuwa na nafasi ya kufanya hivyo,

(iv) kuwa hauhitaji ulinzi wa kimataifa kwa kuwa ulinzi unapatikana kwako katika sehemu ya nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani,

(v) kuwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani ni nchi salama ya asili/nchi ya makazi ya zamani.

iwapo kesi inajumuisha moja kati ya matokeo haya, kipindi kifupi cha kukata rufaa kwa IPAT kinaweza kutumika. Angalia **Sehemu ya 5** ya maelezo kuhusu mchakato wa kukata rufaa.

4.7.3 Kama sehemu ya mchakato mmoja wa utaratibu, ukipatikana haufaii hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala, Waziri anaweza kufikiria kama kuna sababu zozote za kupewa kibali cha kusalia Nchini (Ayalandi). Tafadhali angalia **aya ya 1.6 na sehemu ya 13.**

4.7.4 Waziri atakufahamisha wewe na wakili wako (kama anajulikana) kuhusu mapendekezo ya afisa wa ulinzi wa kimataifa kupitiabarua ya posta. Kama mapendekezo ni ya kuwa unastahili kupewa hadhi ya ukimbizi, utaarifiwa kuhusu maelezo hayo.

Kama utanyimwa hadhi ya ukimbizi au hadhi zote za ukimbizi na hifadhi mbadala, utatumiwa:

(i) taarifa ya sababu za pendekezo hilo,

(ii) nakala ya ripoti yenye pendekezo hilo, na

(iii) maelezo kuhusu jinsi ya kukata rufaa ya pendekezo hili, kwa IPAT.

4.7.5 Ukipatikana kuwa hustahili ulinzi wa kimataifa, utapokea pia uamuzi kama Waziri ameamua kukupa kibali cha kusalia kwa sababu nyingine, utakaoelezea sababu za uamuzi huu.

4.7.6 Unaweza kukata rufaa ya pendekezo la kutokupa ulinzi wa kimataifa (aidha hadhi ya ukimbizi au hadhi zote za ukimbizi na hifadhi mbadala) kwa IPAT. Uamuzi wa IPAT kuhusu rufaa yako, na sababu yake, utawasilishwa kwako na kwa mwakilishi wako wa kisheria (kama anajulikana).

4.7.7 Huweza kukata rufaa ya uamuzi wa Waziri wa kutokupa kibali cha kusalia.

4.7.8 Ukikata rufaa ya pendekezo la kutokupa ulinzi wa kimataifa na IPAT idumishe pendekezo hilo, itabidi Waziri abatilishe uamuzi wa kutokupata kibali cha kusalia ikiwa umewasilisha maelezo yoyote mapya yanayohusiana na mabadiliko ya hali (ambayo ni muhimu kwa uamuzi huo) tangu uamuzi halisi ulipotolewa (angalia **aya ya 13.5**).

## 4.8 4.8 Je, ni nini hufanyika kama sijapokea mapendekezo ya maombi yangu ya ulinzi wa kimataifa katika miezi 6?

4.8.1 Kama hujapokea pendekezo kuhusu maombi yako katika miezi 6, Waziri, kwa ombi lako, atakupa maelezo kuhusu kipindi kinachokadiriwa cha muda ambapo pendekezo litatolewa. Hata hivyo, kadirio hili kivyake halifungi IPO kutoa pendekezo kwa wakati huo.

## Sehemu ya 5
## Rufaa na Ulinzi wa Kimataifa

### 5.1 Je, nina haki ya kukata rufaa ya pendekezo la kutonipa ulinzi wa kimataifa na mapendekezo mengine?

5.1.1 Ndio. Kama imependekezwa kuwa huna haki ya kupata hadhi ya ukimbizi au kuwa huna haki ya kupata hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala unaweza kukata rufaa ya pendekezo hilo.

5.1.2 Pia una haki ya kukata rufaa ya pendekezo ambalo

(i) maombi yako ya ulinzi hayakubaliki, au

(ii) hustahili kuruhusiwa kutuma maombi ya kufuatia ya ulinzi wa kimataifa.

### 5.2 Ninawezaje kukata rufaa?

5.2.1 Ni lazima utume maombi ya rufaa kwa Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa. Wakati unapopokea pendekezo lako utapewa nakala ya fomu ya rufaa ambayo unahitaji kukamilisha.

### 5.3 Je kuna kikomo cha muda wa kuwasilisha maombi ya rufaa?

5.3.1 Maelezo ya kikomo cha muda yatajumuishwa na pendekezo lako.

### 5.4 Je, nina haki ya kupata uwakilishi wa kisheria kwa maombi yangu ya rufaa?

5.4.1 Ndio. Unastahili kujadili maombi yako ya rufaa na mwakilishi wako wa kisheria. Kama huna mwakilishi wa kisheria, unaweza kuwasiliana na Bodi ya Usaidizi wa Kisheria. Vinginevyo, unaweza kumwajiri wakili wa kibinafsi kwa gharama yako ili akusaidie.

### 5.5 Itachukua muda upi kusikiliza maombi yangu ya rufaa?

5.5.1 Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa itawasiliana na wewe na maelezo ya ni lini maombi yako ya rufaa yatasikilizwa.

### 5.6 Ni wapi ninaweza kupata maelezo zaidi kuhusu mchakato wa rufaa?

5.6.1 Maelezo kuhusu mchakato wa maombi ya rufaa kuhusiana na maombi ya ulinzi wa kimataifa yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya IPAT www.protectionappeals.ie.

## Sehemu ya 6
## Taarifa ya Hadhi ya Ukimbizi au Hifadhi Mbadala

### 6.1 Je, ni nini hufanyika baada ya kupokea pendekezo?

6.1.1 Kama IPO itapendekeza kuwa unastahili kupewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala, au IPAT ibatilishe pendekezo linalopinga la IPO, Waziri atakupatia hadhi ya ukimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala haraka iwezekanavyo, yoyote ambayo inatumika. Hii inategemea **aya ya 6.1.4** hapa chini.

6.1.2 Kama IPO itapendekeza kuwa unastahili hadhi yoyote hapa, na

(i) ukose kukata rufaa, au

(ii) ukate rufaa na ushindwe kufanikiwa,

Waziri atakataa kukupa hadhi yoyote hapa.

6.1.3 Hadhi ya ukimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala itakoma kutumika iwapo utakuwa raia wa Ayalandi.

6.1.4 Hata kama IPO itapendekeza au IPAT itaamua kuhusu maombi ya rufaa kwamba wewe ni mkimbizi, huenda Waziri akakataa kukupa hadhi hiyo ikiwa:

(i) kuna sababu zinazoaminika kuhusu wewe kuwa hatari kwa usalama wa Nchi (Ayalandi) au

(ii) wewe ni hatari kwa Jumuia ya Nchi (Ayalandi), ikiwa ulikuwa umehukumiwa kwa uhalifu mbaya (ndani au nje ya Nchi (Ayalandi).

## Sehemu ya 7
## Haki Zako ikiwa Utapewa Ulinzi wa Kimataifa

### 7.1 Je, haki zangu ni zipi kama nitapokea ulinzi wa kimataifa?

7.1.2 Ukipokea hadhi ya ukimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala, kulingana na matoleo ya Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa, 2015, una haki ya:

(i) kutafuta na kufanya kazi, kushiriki katika biashara au kazi yoyote, na kupata elimu na mafunzo Nchini (Ayalandi) kwa njia au hali sawa kama raia wa Ayalandi;

(ii) kupokea, kulingana na hali sawa zinazotumika kwa raia wa Ayalandi, huduma sawa ya kimatibabu na faida sawa za ustawi wa kijamii kama zile raia wa Ayalandi wanazipokea;

(iii) kuishi Nchini (Ayalandi) kwa **kipindi kilichobainishwa** kisichopungua miaka mitatu ambacho kinaweza kubadilishwa kulingana na masharti; na

(iv) kuwa na haki sawa za kusafiri kwenda na kutoka Nchini (Ayalandi) kama za raia wa Ayalandi na hata pia hati ya kusafiri.

# Sehemu ya 8
# Haki na Majukumu Yako katika Mchakato wa Ulinzi wa Kimataifa

## 8.1 Je, haki zangu ni zipi katika mchakato wa maombi ya ulinzi wa kimataifa?

8.1.1 Isipokuwa kesi yako iwe inastahili kushughulikiwa chini ya Kanuni za EU Dublin, ambapo mipango tofauti inatumika (angalia **sehemu ya 10**), haki zako kama mwombaji wa ulinzi wa kimataifa zinajumuisha yafuatayo:

(i) Utapewa kibali na Waziri cha kuingia na kusalia Nchini (Ayalandi) kwa madhumuni ya uchunguzi wa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa na IPO na maombi yako ya rufaa kwa IPAT. Angalia **aya ya 8.1.2.**

(ii) Una haki, ikiwa inafaa na inawezekana, ya kupewa mkalimani ili kuhakikisha mawasiliano yanayostahili.

(iii) Una haki ya kutafuta ushauri na usaidizi wa kisheria kutoka wa Bodi ya Usaidizi wa Kisheria. Vinginevyo, unaweza kutumia uwakilishi wa kisheria wa kibinafsi kwa gharama zako mwenyewe, kama utataka.

(iv) Una haki ya kuwasiliana na UNHCR. Maelezo ya mawasiliano yanaweza kupatikana kwenye **Kiambatisho**.

(v) Una haki ya kuwasilisha maelezo kwa Waziri yanayohusiana na maombi yako. Mawasilisho haya lazima yawasilishwe kwa kuandika.

(vi) Shirika la Mapokezi na Ushirikiano (RIA) linaweza kukupa malazi (na vyakula vyote) wakati maombi yako ya ulinzi yanapokuwa yakichakatwa. Ukubalifu wa toleo hili unategemea wewe kutii Kanuni hizi ambazo zinapatikana kwenye www.ria.ie. Maelezo ya mawasiliano yanaweza kupatikana kwenye **Kiambatisho**.

(vii) Maelezo yote yaliyotolewa kuhusiana na maombi yako yatashughulikiwa kwa siri. Hata hivyo, huenda maelezo yakafichuliwa kwa mashirika mengine ya umma ambayo yanaweza kuwa yanahusika na wewe, kama vile Idara na Mashirika ya Serikali ya Ayalandi ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Uhamiaji, Garda Síochána (Polisi wa Ayalandi) na Serikali za Mitaa. Hii itawezesha mashirika haya kutekeleza kazi zao ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa sheria zinazohusiana na kuingia na kuondoa watu wa kigeni Nchini (Ayalandi). Huenda baadhi ya maelezo haya yakapeanwa kwa nchini nyingine zinazotumia Kanuni za EU Dublini.

(viii) Utaarifiwa kwa kuandikiwa na IPO, IPAT au Waziri, kuhusu miadi, mahojiano, maamuzi au ilani nyingine zozote zinazohusiana na maombi yako ya ulinzi wa kimataifa kwenye anwani uliyotupatia.

8.1.2 Cheti chako cha Makazi ya Muda kitabakia halali hadi ukome kuwa mwombaji wa ulinzi wa kimataifa, kwa mfano wakati Waziri atakataa kukupa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala au kama umehamishwa kutoka Nchini (Ayalandi) kulingana na Kanuni za EU Dublin.

## 8.2 Je, majukumu yangu ni yapi katika mchakato wa maombi ya ulinzi wa kimataifa?

8.2.1 Majukumu yako kama mwombaji wa ulinzi wa kimataifa ni kama yafuatayo:

(i) Lazima utii sheria za Nchi (Ayalandi) na mahitaji mengine ambayo utapewa.

(ii) Ni wajibu wako kushirikiana kikamilifu katika uchunguzi wa hali zote za maombi yako na katika kuamua rufaa yoyote, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha maelezo na hati zote ambazo unazo ili kuunga mkono maombi yako.

(iii) Ukibadilisha anwani yako, **ni lazima uarifu IPO, kwa kuandika**, kuhusu maelezo ya anwani yako mpya **mara moja.** Hii inatumika hata kama umehamishwa hadi kwa makazi mapya na Shirika la Mapokezi na Ushirikiano (RIA). **Kushindwa kufanya hivyo ni makosa.**

(iv) Katika mawasiliano yote na IPO au IPAT **unastahili kuandika wazi jina lako, anwani, uraia na nambari ya Kitambulisho** iliyoonyeshwa kwenye Cheti chako cha Makazi ya muda.

(v) **Hustahili kuondoka au kujaribu kuondoka Nchini (Ayalandi),** bila kibali cha Waziri, wakati maombi yako yanaendelea kuzingatiwa. Kuondoka Nchini (Ayalandi) bila kibali cha Waziri **ni makosa.**

(vi) **Huna haki ya kutafuta, kupata ajira au kushiriki katika biashara au kazi yoyote yenye kipato.** Kufanya kazi au biashara **ni makosa**.

(vii) Wewe au mwakilishi wako wa kisheria lazima **mbakie na nakala zote za hati** ulizopewa na IPO na IPAT.

(viii) **Huenda ukahitajika kuishi na kusalia katika wilaya au mahali fulani** Nchini (Ayalandi) Kushindwa kufanya hivyo **ni makosa.**

(ix) **Huenda ukahitajika kuripoti mara kwa mara** kwa Afisa wa Uhamiaji, au katika kituo maalum cha Garda Síochána (Polisi wa Ayalandi). Kushindwa kufanya hivyo **ni makosa.**

(x) Lazima uwe **mkweli** wakati wote katika maelezo unayotoa kuhusiana na maombi yako na kushindwa kufanya hivyo **ni makosa.**

(xi) Unastahili kuwasilisha katika dodoso lako maelezo yoyote ambayo unayo ambayo ni muhimu kwa uamuzi wa Waziri wa kukupa au kukunyima kibali cha kusalia. Unaweza pia kuwasilisha maelezo yoyote ambayo yanaweza kuwa muhimu kwa uamuzi wa Waziri kuhusu kukupa kibali cha kusalia wakati wa kipindi kati ya kutuma maombi yako na maandalizi ya ripoti kuhusu uchunguzi wa maombi yako ya ulinzi. Unastahili pia kumjulisha Waziri kuhusu mabadiliko yoyote ya hali ambazo zinaweza kuwa muhimu kwa uamuzi wa Waziri kuhusu suala hila mara moja. Maelezo kuhusu kibali cha kusalia yanaweza kupatikana katika **sehemu ya 13**.

(xii) Unastahili kuwasilisha maelezo yote muhimu ambayo unayo au kudhibiti kwa IPO au IPAT haraka iwezekanavyo.

**MUHIMU**

**8.2.2** Unastahili kupatia IPO au IPAT (inayofaa) **maelezo kuhusu uwakilishi wako wa kisheria (jina, anwani, nambari ya simu n.k.) na mabadiliko yoyote ya ushauri wa kisheria haraka iwezekanavyo**. Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kuhatarisha uwezo wako wa kupokea ushauri na usaidizi kutoka kwa mwakilishi wako wa kisheria kuhusu mawasiliano na maamuzi kuhusiana na maombi yako ya ulinzi wa kimataifa.

## Sehemu ya 9
## Watoto Wasiokuwa na Wazazi

### 9.1 Je, ni nini hufanyika nikitafuta kuomba ulinzi wa kimataifa kama mtoto asiyekuwa na wazazi?

9.1.1 Iwapo unachukuliwa kuwa mtoto (chini ya umri wa miaka 18), na huna mtu mzima anayekulea au kukulinda, utaelekezwa kwa TUSLA - Shirika la Watoto na Familia.

9.1.2 Huenda ukahitajika kufanya mahojiano ya utathmini wa umri utakaotekelezwa na IPO. Mahojiano ya kutathmini umri yameundwa ili kubainisha ukweli wa mambo kuhusu mipango yako ya kusafiri, maelezo kuhusu wazazi wako, kiwango chako cha elimu na kiwango cha kukomaa. Kisha afisa anayetekeleza mahojiano ataamua kama anafikiria wewe una umri chini ya miaka 18 k**wa usaidizi wa TUSLA - Shirika la Watoto na Familia kama itahitajika.**

9.1.3 Kama umeelekezwa na TUSLA - Shirika la Watoto na Familia, shirika hilo litawajibika kwa ajili yako na kuamua kama ni vyema kwako kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa au kama kuna chaguo nyingine zinazotumika kama vile kuungana na familia au kutafuta familia.

### 9.2 Je, ni utaratibu upi kama TUSLA - Shirika la Watoto na Familia litatuma maombi ya ulinzi wa kimataifa kwa niaba yangu?

9.2.1 Kama TUSLA - Shirika la Watoto na Familia litaamua kwamba ni kwa manufaa yako kutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa kwa niaba yako, kwa misingi ya maelezo pamoja na ushauri wa kisheria unaopatikana kwa ajili yako, shirika hili litapanga mkutano na mwajiri wa TUSLA - Wakala wa Watoto na Familia, au watu wengine kama hao kama itakavyoamua, ili kutuma maombi kama hayo na kukuwakilisha na kukusaidia katika mahojiano na mchakato wa uchunguzi.

### 9.3 Je, ni utaratibu upi unaotumiwa kumwelekeza mtoto chini ya umri wa miaka 18 kwa Bodi ya Usaidizi wa Kisheria?

9.3.1 TUSLA - Shirika la Watoto na Familia linaweza kuwasiliana na LAB ili kupanga uwakilishi wa kisheria kwa niaba yako. Mipango maalum itafanywa na TUSLA - Shirika la Watoto na Familia kukuzindikisha kwa mahojiano yako.

# Sehemu ya 10
# Kanuni za EU Dublin

## 10.1 Je, Kanuni za EU Dublin ni nini?

10.1.1 Kanuni za EU Dublin hutoa misingi ya kisheria na kanuni za utaratibu za kuamua kigezo na mbinu za kubainisha nchi inayowajibika kuchunguza maombi ya ulinzi wa kimataifa yaliyotumwa katika moja ya nchi husika na mtu wa nchi nyingine au mtu asiyekuwa na taifa.

10.1.2 Wakati unapotuma ombi la ulinzi wa kimataifa kwa IPO, utapewa maelezo zaidi kuhusu mchakato wa Dublin.

10.1.3 Kama matokeo ya Kanuni za EU Dublin zitatumika kwako unaweza kuhamishwa kwa nchi nyingine inayohusika ili kuchunguza maombi yako ya ulinzi wa kimataifa huko.

## Sehemu ya 11
## Chaguo za Kurejea kwa Hiari

### 11.1 Je, nina chaguo la kurejea nchi yangu ya asili/nchi ya makazi yangu ya zamani kwa hiari?

11.1.1 Chaguo ambalo linapatikana kwako wakati wowote wa uchunguzi wa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa au baada ya kunyimwa maombi yako ni kurejea kwa hiari kwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani. Kama maombi yako ya ulinzi yataondolewa, utakuwa pia na chaguo wakati huo la kurejea kwa hiari kwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi yako ya awali.

11.1.2 Kama Waziri atakuarifu kuhusu uamuzi wake wa kukataa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa utaarifiwa kuhusu chaguo la kurejea nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani. Ili kupata chaguo hili wakati huo, lazima umwarifu Waziri kwa kumwandikia ndani ya siku tano kuanzia tarehe ya taarifa ya Waziri. Barua ya uamuzi wako itakupa maelezo ya ni nani unayestahili kuwasiliana na yeye ili kupanga kurejea kwako kwa hiari kwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani.

11.1.3 Kama utaamua kurejea kwa hiari katika nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani, utaweza kupata ushauri na usaidizi kutoka kwa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM). Tafadhali angalia **Kiambatisho** kwa maelezo ya mawasiliano.

11.1.4 IOM inaweza kukusaidia kupata hati zinazostahili za kusafiri, na hata pia kushughulikia gharama za kifedha za safari yako kutoka Ayalandi hadi nchi yako ya asili. Licha ya hayo, ruzuku ndogo ya ushirikiano inapatikana kwa watu wote wanaorejea ili kusimamia gharama za shughuli za kuzalisha kipato, kama vile elimu, mafunzo ya kitaalamu na/au kuanzisha biashara.

11.1.5 Kama utaamua kutofuatilia chaguo la kurejea kwa hiari kwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani, Waziri ataendelea kukupa amri ya kufukuzwa nchini na mipango itafanywa ya kukuondoa Nchini (Ayalandi). Kama hutatii amri ya kufukuzwa nchini, hutakuwa na msingi wowote wa kisheria wa kusalia Nchini (Ayalandi).

11.1.6 Idara ya Haki na Usawa huwasaidia watu moja kwa moja ambao wangependa kurejea kwa hiari kwa nchi zao za asili/nchi ya makazi ya zamani kwa kuwapa usaidizi wa usimamizi na usaidizi zaidi kwa watu wanaoomba usaidizi.

11.1.7 Faida za kutumia chaguo hili la kurejea kwa hiari kwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya asili ni kuwa mipango kama hiyo hukuwezesha kurejea Nchini (Ayalandi) baadaye kama utakuwa na sababu za kisheria za kufanya hivyo. Upande ule mwingine, mtu ambaye atalazimika kufukuzwa nchini anastahili kisheria kuondoka Nchini (Ayalandi) na kubaki nje ya Nchi (Ayalandi) (isipokuwa amri ya kufukuzwa nchini ibatilishwe).

## Sehemu ya 12
## Maelezo Mengine

### 12.1 Je, ni taratibu zipi zinazotumika za kuipa kipaumbele maombi ya ulinzi wa kimataifa?

12.1.1 Huenda Waziri akaipa kipaumbele maombi yoyote ya ulinzi wa kimataifa ambapo Waziri atafikiria ni muhimu kufanya hivyo kulingana na mahitaji ya haki na utendaji wa kushughulikia maombi kama hayo ya ulinzi wa kimataifa.

12.1.2 Katika kuipa kipaumbele, Waziri anaweza kuzingatia yafuatayo:

(i) Kama mwombaji ana hati za utambulisho, na kama hana, kama anaweza kutoa ufafanuzi mwafaka wa kukosa hati hizo.

(ii) Kama mwombaji ametoa ufafanuzi mwafaka wa kuthibitisha madai yake kuwa Nchi (Ayalandi) ni nchi salama ya kwanza ambayo aliwasili tangu kutoka nchi yake ya asili/nchi ya makazi ya zamani;

(iii) Kama mwombaji ametoa ufafanuzi kamili na wa kweli wa jinsi alivyosafiri na kuwasili Nchini (Ayalandi).

(iv) Ikiwa maombi yalitumwa mahali pengine kando na mpaka wa Nchi (Ayalandi), kama mwombaji ametoa ufafanuzi mwafaka wa kuonyesha ni kwanini hakutuma maombi ya ulinzi wa kimataifa, au kulingana na kesi, maombi chini ya sehemu ya 8 ya Sheria ya Wakimbizi ya 1996 mara moja alipowasili mpakani wa Nchi (Ayalandi) isipokuwa maombi hayo yawe yanategemea matukio ambayo yamefanyika tangu alipowasili Nchini (Ayalandi).

(v) Kama mwombaji ameghushi, kuharibu au kutupa kitambulisho chochote au hati nyingine muhimu kwa maombi yake, awe ana ufafanuzi mwafaka wa kufanya hivyo au la.

(vi) Kama mwombaji ametoa ushahidi wa uongo wa kuunga mkono maombi yake, au amewasilisha hati za uongo, kwa kusema au kwa kuandika.

(vii) Kama mwombaji, bila sababu nzuri, ametuma maombi kufuatia taarifa ya pendekezo la kumfukuza Nchini (Ayalandi).

(viii) Kama mwombaji ametimiza wajibu wake wa kushirikiana na mchakato wa ulinzi.

(ix) Kama mwombaji ni mtu ambaye anahudumiwa na kulindwa na TUSLA - Shirika la Watoto na Familia.

(x) Kama mwombaji, kwa sababu nzuri, ameshindwa kutimiza mahitaji mengine yanayohusishwa na kibali chake cha kuingia na kusalia Nchini (Ayalandi).

## 12.2 Je, ni nini kitakachofanyika kwa maelezo ninayoyatoa kwa Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa?

12.2.1 Wakati unapotoa maelezo yako ya kibinafsi kwa IPO, kuna wajibu wa ofisi wa kuweka maelezo yako siri na salama.

12.2.2 Una haki ya kupata, kusahihisha na kufuta maelezo ya kibinafsi ambayo tunayo, kulingana na haki zako chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data ya 1988 na 2003.

12.2.3 Taarifa zinazohusiana na maelezo ya kibinafsi zinazomilikiwa na Huduma ya Uraia na Uhamiaji katika mpangilio wa Sheria ya Uhuru wa Habari ya 2014, kwa kutegemea misamaha fulani.

12.2.4 Sheria ya Uhuru wa Habari ya 2014 imebainisha haki ya kisheria ya kila mtu ya:

(i) Kupata maelezo yanayomilikiwa na vyombo vya umma.

(ii) Kurekebisha maelezo rasmi yanayohusiana naye ikiwa si kamili, sahihi au yanapotosha.

(iii) Kupata ufafanuzi wa sababu za maamuzi yanayomwathiri.

12.2.5 Sheria ya 2014 inathibitisha haki ya umma ya kupata maelezo rasmi yanayolingana na maslahi ya umma na haki ya faragha ya watu.

12.2.6 Tafadhali angalia tovuti ya IPO www.ipo.gov.ie kwa maelezo zaidi kuhusu Ulinzi wa Data.

# Sehemu ya 13
# Kibali cha Kusalia

## 13.1 Ninawezaje kuomba kibali cha kusalia?

13.1.1 Wakati unapotuma maombi yako ya ulinzi wa kimataifa lazima kwa wakati huo uwasilishe maelezo yoyote ambayo unaweza kuwa nayo ambayo ni muhimu kwa uamuzi wa Waziri wa kama atakupa kibali cha kusalia, kama hutapewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala. Kama kuna kitu chochote unachotaka Waziri akizingatie, lazima uhakikishe umefahamisha IPO kukihusu haraka uwezavyo.

13.1.2 Unahitajika kutoa maelezo haya katika sehemu inayofaa ya dodoso lako la ulinzi wa kimataifa. Unastahili kutoa hati zozote saidizi ambazo unadhania ni muhimu (kwa mfano, vyeti vya kuzaliwa au ndoa, hati za mwenendo wako, ushahidi au stakabadhi za kuhitimu, n.k.) Kama huna hati hizi, unaweza kuziwasilisha baadaye, wakati wowote ule hadi wakati IPO itaanda taarifa kwa Waziri kuhusu maoni yako ya ulinzi wa kimataifa.

13.1.3 Licha ya hayo, unastahili kutoa maelezo yaliyosasishwa kwa IPO kama kuna mabadiliko yoyote katika hali yako ambayo ni muhimu kwa uamuzi wa Waziri wa kibali cha kusalia.

13.1.4 Tafadhali kumbuka kwamba mahojiano ambayo yatatekelezwa na IPO yanalenga kuchunguza maombi yako ya ulinzi wa kimataifa na wala sio kibali cha kusalia. Afisa wa kuhoji atakuuliza maswali yanayohusiana na ulinzi wa kimataifa na hatauliza kuhusu mambo mengine, ijapokuwa si muhimu kwa maombi yako ya ulinzi, huenda yakawa muhimu kwa uamuzi wa Waziri wa kukupa au kukunyima kibali cha kusalia Nchini (Ayalandi). Hata hivyo, kama masuala kama hayo yataibuka, yataandikwa na mhoji na yataweza kuzingatiwa na Waziri katika kuamua kama atakupa kibali cha kusalia kama hutapewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala.

## 13.2 Ni maelezo gani muhimu kwa uamuzi wa Waziri kama atanipa au hatanipa kibali cha Kusalia Nchini (Ayalandi)?

13.2.1 Waziri atazingatia maelezo yoyote muhimu yaliyowasilishwa na wewe ikiwa ni pamoja na maelezo muhimu yaliyowasilishwa kwenye maombi yako ya ulinzi wa kimataifa na taarifa yoyote uliyoiwasilisha katika mahojiano yako ya mwanzo na mahojiano yako ya kibinafsi ya ulinzi wa kimataifa.

13.2.2 Lazima Waziri azingatie hali za familia yako na za kibinafsi na haki yako ya kuheshimu maisha yako ya kibinafsi na ya familia, na kuheshimu:

(i) hali ya mahusiano yako na Nchi (Ayalandi)

(ii) masuala ya kibinadamu,

(iii) tabia na mienendo yako ndani na nje ya Nchi (Ayalandi) (ikiwa ni pamoja na hukumu za uhalifu),

(iv) masuala ya usalama wa taifa na umma, na

(v) masuala mengine yanayowafaidi watu wote.

13.2.3 Waziri atazingatia pia masuala yoyote yaliyoibuliwa na wewe kuhusu makatazo ya kurejeshwa nchi ya nyumbani (angalia **aya ya 2.7.1**).

### 13.3 Ni nini hufanyika kama nitanyimwa kibali cha kusalia?

13.3.1 Kama utaamua kutokata rufaa pendekezo kuhusu maombi yako ya ulinzi kwa IPAT, na Waziri akunyime kibali cha kusalia, basi hutaweza kusalia Nchini (Ayalandi). TRC yako haitakuwa halali tena na ni lazima urejeshe cheti hicho kwa IPO mara moja.

13.3.2 Utakuwa na chaguo la kurejea kwa hiari katika nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani na lazima huarifu IPO na INIS kama utaamua kuondoka Nchini (Ayalandi) kwa hiari.

13.3.3 Ukiamua kutorejea kwa hiari kwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani, Waziri atatoa Amri ya kufukuzwa Nchini itakayokuhitaji uondoke Ayalandi na ubakie nje ya Nchi hii milele.

### 13.4 Ni nini hufanyika kama nitapewa kibali cha kusalia?

13.4.1 Kama utapewa kibali cha kusalia utapokea barua inayokupa maelezo ya kina kuhusu hatua unazostahili kuchukua na haki na majukumu yako.

### 13.5 Je "mapitio" ya kunyimwa kibali cha kusalia hufanya kazi aje?

13.5.1 Huwezi kukata rufaa ya uamuzi wa kukunyima kibali cha kusalia.

13.5.2 Kama utanyimwa pendekezo linalohusiana na ulinzi wa kimataifa na IPO, utapokea maelezo kuhusu mchakato wa maombi ya rufaa kwa IPAT. Kama utakata rufaa kwa IPAT lakini ithibitishe pendekezo usilopenda la IPO, utapokea fomu ya *Mapitio ya Kibali cha Kusalia* ili ukamilishe. Kipindi cha muda wa kukamilisha na kurejesha fomu hii kitatolewa kwako pamoja na fomu.

13.5.3 Kama hali zako zitabadilika katika kipindi kati ya kibali cha kwanza cha uamuzi wa Waziri wa kusalia na uamuzi wa IPAT kuhusu rufaa yako ya ulinzi wa kimataifa, kwa njia ambayo ni muhimu kwa uamuzi wa kwanza wa Waziri, unastahili kumfahamisha Waziri kuihusu punde tu ukijua.

13.5.4 Kama umewasilisha maelezo yoyote muhimu kwa uamuzi wa kibali cha kwanza cha kusalia cha Waziri yakiashiria mabadiliko ya hali, Waziri atapitia uamuzi wake wa awali wa kukunyima kibali cha kusalia. Waziri atazingatia tena masuala yaliyoorodheshwa katika **aya ya 13.2.2** hapa juu na maelezo yoyote ya ziada yaliyowasilishwa na wewe. Waziri atazingatia pia masuala yoyote yaliyoibuliwa na wewe kuhusu makatazo ya kurejeshwa nchi ya nyumbani.

13.5.5 Kufuatia mapitio ya uamuzi wa kibali chako cha kusalia, Waziri anaweza kukupa kibali cha muda cha kusalia kwa kipindi cha muda fulani au akatae kukupa kibali hicho. Utafahamishwa kwa kuandikiwa kuhusu uamuzi wa Waziri na sababu za uamuzi huo.

## 13.6 Je, ni nini hufanyika kama nitapewa kibali cha kusalia lakini niamue kukata rufaa pendekezo hilo la ulinzi kutoka kwa IPO hadi kwa IPAT?

13.6.1 Unaweza bado kujiandikisha kwenye Ofisi ya Usajili ya Uhamiaji katika eneo lako ili kibali chako cha kusalia Nchini (Ayalandi) kiweze kutekelezwa. Hata hivyo, kama utakata rufaa ya uamuzi wa ulinzi, kwa sababu bado wewe ni mwombaji wa ulinzi wa kimataifa, hutaweza kuajiriwa, kuhusika katika biashara au kazi yoyote hadi matokeo ya rufaa yako kwa IPAT yajulikane.

## 13.7 Ni nini hufanyika kama nitanyimwa kibali cha kusalia baada ya mchakato wa mapitio?

13.7.1 Kama umenyimwa kibali cha kusalia, hutaweza tena kusalia Nchini (Ayalandi). TRC yako haitakuwa halali tena na ni lazima urejeshe cheti hicho kwa IPO mara moja.

13.7.2 Utakuwa na chaguo la kurejea kwa hiari katika nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani na lazima huarifu IPO na INIS kama utaamua kuondoka Nchini (Ayalandi) kwa hiari.

13.7.3 Ukiamua kutorejea kwa hiari kwa nchi yako ya asili/nchi ya makazi ya zamani, Waziri atatoa Amri ya kufukuzwa Nchini itakayokuhitaji uondoke Nchini (Ayalandi) na ubakie nje ya Nchi hii (Ayalandi) milele.

## Sehemu ya 14
## Kuungana na Familia

### 14.1 Je, kuungana na Familia ni nini?

14.1.1 Kama Waziri atakupa hadhi ya ukimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala, unaweza katika miezi 12 kuanzia tarehe ya hadhi hiyo, kuomba Waziri kibali cha wanafamilia **fulani**

- kuingia na kuishi Nchini (Ayalandi), ikiwa wako nje wakati wa maombi; au
- kusalia na kuishi Nchini (Ayalandi), ikiwa tayari wako Nchini (Ayalandi) wakati wa maombi.

### 14.2 Je, kuna kikomo cha muda?

14.2.1 Lazima uwasilishe maombi ya wanafamilia wako kujiunga na wewe ndani ya **miezi 12** ya kupewa hadhi ya ukimbizi au hadhi ya hifadhi mbadala.

### 14.3 Mwanafamilia ni nani?

14.3.1 **Mwanafamilia** ameelezewa kwa undani. Humaanisha:

(i) Mwanandoa wa mtu aliye nchini (Ayalandi), bora ndoa hiyo ilikuwa kabla ya tarehe ya maombi ya ulinzi wa kimataifa,

(ii) Mpenzi anayetambuliwa na serikali wa mtu aliye nchini (Ayalandi), bora uhusiano huo ulikuwa kabla ya tarehe ya maombi ya ulinzi wa kimataifa

(iii) Kama mtu huyo yuko chini ya umri wa miaka 18 na hajaolewa, wazazi wake na watoto wake ambao wako chini ya umri wa miaka 18 na hawajaolewa, au

(iv) Mtoto ambaye, siku ya maombi ya kuungana na familia, yuko chini ya umri wa umri wa miaka 18 na hajaolewa.

### 14.4 Ni maelezo gani ambayo ni lazima niyajumuishe kwenye Fomu ya Maombi ya Ulinzi wa Kimataifa na Dodoso?

14.4.1 Wakati unaomba ulinzi wa kimataifa, utahitajika kutoa maelezo muhimu kuhusu wanafamilia ambao, iwapo utapewa ulinzi wa kimataifa, wanastahili kuungana na familia (angalia **aya ya 14.3**).

14.4.2 Lazima utoe maelezo muhimu kuhusu wanafamilia wako kwenye Dodoso la Ulinzi wa Kimataifa.

14.4.3 Ni muhimu sana kwako kujumuisha maelezo yote ya wanafamilia wako wakati unapokuwa ukikamilisha maombi na dodoso yako, na kutoa hati muhimu kama vile vyeti vya ndoa, vyeti vya kuzaliwa, n.k.

### 14.5 Ninawezaje kuomba kuungana na familia?

14.5.1 Kama umepewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala na ungependa kuomba kuungana na familia kwa mwanafamilia aliyerejelewa kwenye **aya ya 14.3**, unastahili kuomba kwa kuandika kwa Kitengo cha Kuungana na Familia (INIS) kwenye anwani ifuatayo:

**Family Reunification Unit**
**Irish Naturalisation and Immigration Service**
**13/14 Burgh Quay**
**Dublin 2**
**D02 XK70**

14.5.2 Maelezo zaidi yanapatikana kwenye www.inis.gov.ie

**KUMBUKA KUWA MAOMBI YA KUUNGANA NA FAMILIA YANASTAHILI KUWASILISHWA KATIKA MIEZI 12 YA KUPEWA HADHI YA UKIMBIZI AU HIFADHI MBADALA.**

# Sehemu ya 15
# Malazi Yako

## 15.1 Maelezo ya Mapokezi/Malezi

15.1.1 Kama umeomba ulinzi wa kimataifa kwa IPO, maelezo yako ya kwanza yatachakatwa kisha utaelekezwa kwa Shirika la Mapokezi na Ushirikiano (RIA) wanaodhibiti masuala yote yanayohusiana na malazi na vyakula vinavyotolewa na Serikali kwa wale walio katika mchakato wa ulinzi wa kimataifa.

15.1.2 Kama unahitaji malazi maelezo yako yatachukuliwa na unaweza kupewa nafasi ya makazi. Ukikubali nafasi hii, utapewa usafiri hadi kwa Kituo cha Mapokezi ambapo utaishi kwa muda wa kipindi kifupi - kwa kawaida huwa chini ya wiki tatu.

15.1.3 Baada ya kipindi kifupi katika Kituo cha mapokezi unaweza kuhamishwa hadi kwenye kituo cha malazi. Hutapewa chaguo lolote kuhusu eneo ka kituo ambacho unahamishwa.

15.1.5 Unaweza kusalia katika kituo cha makazi ambacho ulihamishwa hadi maombi yako ya ulinzi wa kimataifa yachakatwe kikamilifu (ikiwa ni pamoja na maombi yoyote ya rufaa, kama yanahusika) au njia nyingine unaweza kuamua kuishi katika malazi ya kibinafsi kwa gharama yako mwenyewe.

15.1.6 Tafadhali kumbuka kuwa kama utapanga mipango yako mwenyewe ya malazi n.k., una wajibu wa kufahamisha IPO kuhusu mahali uliko.

15.1.7 Nafasi ya malazi katika Kituo cha Mapokezi au Kituo cha Malazi inategemea kama utatii kila wakati Sheria husika katika kituo hicho.

15.1.8 Unaweza kutafuta uhamisho kutoka kwa makazi yaliyotolewa kirasmi kupitia RIA na katika hali ambazo Shirika linaweza kukupa malazi mbadala.

15.1.9 Maelezo zaidi yanaweza kupatikana kutoka kwa Shirika la Mapokezi na Ushirikiano kwenye www.ria.gov.ie .

**KIAMBATISHO**

**MAELEZO YA MAWASILIANO**

**SERIKALI NA MASHIRIKA MENGINE AMBAYO UNAWEZA KUWA UNAWASILIANA NAYO KUHUSIANA NA MAOMBI YAKO YA ULINZI:**

| **Shirika** | **Kazi** |
|---|---|
| Irish Naturalisation and Immigration Service,<br>Department of Justice and Equality.<br>13 – 14 Burgh Quay,<br>Dublin 2.<br>D02 XK70<br><br>Simu: +353 1 616 7700<br>Simu ya bei nafuu:1890 551 500<br>tovuti: www.inis.gov.ie | Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi (INIS) inawajibika katika kutekeleza kazi za usimamizi za Waziri wa Haki na Usawa kuhusiana na hifadhi, uhamiaji (pamoja na visa) na masuala ya raia. INIS husaidia pia serikali katika masuala yote ya uhamisho na hifadhi, ambayo huwezesha huduma inayofaa zaidi katika maeneo haya. |
| International Protection Office<br>Irish Naturalisation and Immigration Service,<br>79-83 Lower Mount Street,<br>Dublin 2.<br>D02 ND99<br><br>Simu: +353 1 602 8000<br>Faksi: + 353 1 602 8122<br>Barua pepe: info@ipo.gov.ie<br>Tovuti: www.ipo.gov.ie | Kazi kuu ya Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO), kati ya mambo mengine, ni kutoa mapendekezo kulingana na matoleo ya Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015 kama mtu ana haki ya ulinzi wa kitaifa Nchini (Ayalandi). Kama mwomba ulinzi hana haki, IPO huzingatia pia kama anastahili kuruhusiwa kusalia Nchini (Ayalandi) kwa sababu nyingine na hata pia kwa kuzingatia makatazo ya kurejeshwa nchi ya nyumbani n.k. |
| International Protection Appeals Tribunal<br>6/7 Hanover Street,<br>Dublin 2.<br>D02 W320<br><br>Simu: +353 1 474 8400<br>Simu ya Bei nafuu: 1890 210 458<br>Faksi: +353 1 474 8410<br>Barua pepe: info@protectionappeals.ie<br>Tovuti: www.protectionappeals.ie | Kazi kuu ya Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa (IPAT) ni kuamua maombi ya rufaa dhidi ya mapendezo yanayopinga ya IPO. Maombi ya rufaa hushughulikiwa na nwanachama wa IPAT. |

| **Shirika** | **Kazi** |
|---|---|
| Reception and Integration Agency.<br>P.O. Box 11487<br>Dublin 2.<br><br>Simu: + 353 1 418 3200<br>Faksi: +353 1 4183271<br>Barua pepe: RIA_Inbox@justice.ie<br>Tovuti: www.ria.gov.ie | Shirika la Mapokezi na Ushirikano (RIA) linajukumu la kupanga malazi na huduma husika zinazotolewa kwa waomba ulinzi. Huduma hizi zinajumuisha matoleo ya malazi, huduma ya afya, elimu na maslahi ya waomba ulinzi. |
| United Nations High Commissioner for Refugees.<br>102 Pembroke Road,<br>Ballsbridge,<br>Dublin 4.<br>D04 E7N6<br><br>Simu: 01 631 4510<br>Tovuti: www.unhcr.org | Tume ya Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa (UNHCR) ilianzishwa mwaka wa 1951 ili kulinda masuala ya wakimbizi. Kazi ya UNHCR imefafanulia kama ya ufadhili, jamii, na isio ya kisiasa. Kazi zake kuu ni kutoa ulinzi wa kimataifa kwa wakimbizi, wanaotafuta suluhisho za kudumu za matatizo yo na kuwapa usaidizi. Ulinzi uhusisha kuzuia kurejeshwa nchi ya nyumbani k.m. mkimbizi kurejeshwa kwa lazima katika nchi ambayo ana sababu za kuhofia mateso. Utaratibu umewekwa wa kufahamisha UNHCR kuhusu mchakato wa maombi kuanzia hatua ya kwanza na ya rufaa. Huenda UNHCR ikahudhuria mahojiano au maombi yoyote ya rufaa au kuwasilisha maelezo yaliyoandikwa kuhusu maombi yoyote |
| International Organisation for Migration.<br>116 Lower Baggot Street,<br>Dublin 2.<br>D02 R252<br><br>Simu bila malipo: 1800 406 406<br>Simu: +353 1 676 0655<br>Barua pepe: iomdublin@iom.int<br>Tovuti: www.ireland.iom.int/ | Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) hutoa usaidizi wa faragha kwa watafuta hifadhi na wahamiaji wasio wa kawaida kutoka Eneo la Kiuchumi lisilo la Ulaya (EEA) ambao wanataka kurejea kwa hiari kwa nchi yao ya nyumbani na hawana njia au hati za kufanya hivyo. |

| Shirika | Kazi |
|---|---|
| Legal Aid Board (Smithfield).<br>48/49 North Brunswick Street,<br>Georges Lane,<br>Dublin 7.<br>D07 PE0C<br><br>Simu: (01) 646 9600<br>Faksi: (01) 671 0200<br>Barua<br>pepe:lawcentresmithfield@legalaidboard.ie<br><br>Legal Aid Board (Cork)<br>Popes Quay Law Centre,<br>North Quay House,<br>Popes Quay,<br>Cork<br>T23 TV0C<br><br>Simu: + 353 21 455 16 86<br>Faksi: +353 21 455 1690<br>Barua<br>pepe:lawcentrecorknorth@legalaidboard.ie<br><br>Galway Law Centre (Seville House)<br>Seville House<br>New Dock Road<br>Galway<br>H91 CKVO<br>Simu: +353 91 562 480<br>Faksi: +353 91 562 599<br>Barua<br>pepe:lawcentresevillehouse@legalaidboard.ie | Waomba ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi wanaweza kuomba usaidizi na ushauri wa kisheria ili kuwasaidia na maombi yao ya ulinzi na rufaa yoyote, kama itahitajika kwa Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa. |
| Team for Separated Children Seeking Asylum,<br>TUSLA- Child and Family Agency<br>Sir Patrick Dun's Hospital,<br>Lower Grand Canal Street,<br>Dublin 2.<br>D02 P667<br><br>Simu: +353 1 647 7000<br>Faksi: +353 1 647 7008<br>Tovuti: www.tusla.ie | TUSLA - Shirika la Watoto na Familia lina wajibu wa mahitaji ya haraka na yanayoendelea ya watoto waliotenganishwa wanaotafuta ulinzi wa kimataifa katika masuala kama vile malezi, matibabu na mahitaji ya umma. |

| **Shirika** | **Kazi** |
| --- | --- |
| The Irish Red Cross Society.<br>16 Merrion Square North,<br>Dublin 2.<br>D02 XF85<br><br>Simu: +353 1 642 4600<br>Faksi: +353 1 661 4461<br>Barua pepe: info@redcross.ie<br>http://www.redcross.ie | Shirika la Msalaba Mwekundu la Ayalandi limejitolea kutoa msaada wa dharura na wa ufadhili kupitia mitandao ya watu wanaojitolea hapa nchini na kimataifa. |